

**ARSENAL IMEJIFUNZA KWA MAKOSA – ARTETA**

UKURASA 21

**POSTA,** TTCL hoi kifedha, wabunge waomba 'zibebwe' deni la mabilioni

UKURASA 2



**ALIYESAIDIWA** vyerehani, ampa ofa Rais Samia kumshonea nguo

UKURASA 3

**FOLENI** meli za mafuta Bandari ya Dar zapigiwa kelele bungeni

UKURASA 4


# Nipashe

Jumanne Februari 6, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 ◦ No. 0581578

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


## KINANA VS CHADEMA

# Lema aibuka, wadau katika hoja kinzani

UKURASA 2



"Anachojaribu kusema Kinana ni vitu ambavyo havina maana, suala la Katiba Mpya si la CCM... walikataa mapendekezo yetu kwa maandishi." **GODBLESS LEMA**

"Tume itakayotokana na miswada hiyo, haiwezi kutibu matatizo ya kiuchaguzi ambayo yamekuwa chanzo cha mazungumzo kati ya CCM na CHADEMA." **ANANILEA NKYA**





"CHADEMA wajitathmini. Kuna haja wakae na kutazama hoja 11 na kuona ni zipi zilizokubaliwa waende nazo na ambazo bado wajipe muda ili zipatiwe ufumbuzi." **ABBAS MWALIMU**

# Mabingwa: Dawa P2 chanzo ujauzito tata na kuharibu hedhi

UKURASA 15



UKURASA WA 4

### MARADHI YA FIGO MAKONDA ASHANGAA MKOA HAUNA HUDUMA

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ameshangaa kukosekana jengo la matibabu ya kusafisha damu wagonjwa wa figo mkoani Katavi licha ya serikali kutoa vifaa kwa ajili ya huduma hiyo...

UKURASA WA 8

### WALIMU NA WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WAPEWA VIFAA SAIDIZI

WALIMU na wanafunzi wenye ulemavu katika Shule za Msingi Mzambarauni, Uhuru Mchanganyiko, Sekondari za Pugu, Benjamin Mkapa na Jangwani jijini Dar es Salaam, zimepatiwa msaada wa vifaa saidizi na Benki ya NMB.
Makabidhiano ya vifaa hivyo...

UKURASA WA 24

### SIMBA KUWASHANGAZA TABORA UNITED NYUMBANI




KOCHA msaidizi wa Simba, Seleman Matola, amesema licha ya kufahamu kuwa mchezo wao wa leo dhidi ya wenyeji wao Tabora United kutarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani...

# Hospitali Temeke yaanzisha huduma ya kushuhudia mwenza akijifungua

UKURASA 3

**MICHEZO** SERENGETI GIRLS YANOA MAKALI 'KUPINDUA MEZA' UK. 23 **KATUNI** UK. 6



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akisalimiana na Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) anayeshughulikia nishati, Dk. Kevin Kariuki, baada ya mkutano wao kuhusu fursa za uwekezaji katika sekta ya nishati, ujenzi wa reli ya kisasa – SGR wa kikanda, jijini Dodoma jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

KINANA vs CHADEMA

# Lema aibuka, wadau katika hoja kinzani

**Na Maulid Mmbaga**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, amejibu hoja zilizoibuliwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana.

Juzi, akizungumza na wanachama wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam katika mkutano maalum, Kinana alitaja sababu zilizokwamisha maridhiano kati yao na CHADEMA, akikinyooshea kidole chama hicho cha upinzani kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo kutokuweka wazi kwamba kimepewa na serikali ruzuku ya Sh. bilioni 2.7 kiliyoikataa awali.

Katika kujibu hoja hizo za Kinana jana jijini Arusha, Lema aliyekuwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Serengeti, John Heche, alisema kuwa katika vikao vya maridhiano na CCM, waliwasilisha hoja zote alizozitaja Kinana juzi, ikiwamo kudai utawala bora, mabadiliko ya Katiba ya nchi na kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi.

Alisema hoja hizo pamoja na madai ya kuwaondoa bungeni wabunge 19 waliovuliwa uanachama wa CHADEMA, ziliwasilishwa kwa maandishi na zilijibiwa na CCM kwa maandishi.

Lema aliyekimbilia ughaibuni baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 kutokana na hofu ya usalama wake, alisisitiza wabunge hao 19 wanachukua fedha za serikali kinyume cha sheria kwa kuwa tayari Mahakama Kuu ilishatamka uamuzi wa kuvuliwa uanachama wa CHADEMA haukuwa na dosari kisheria.

"Kinana jana hajaongea, ila ame... (alitamka neno lenye maana ya kusema maneno mengi yasiyokuwa na maana). Na mimi nilipoona nilijua labda si sauti yake, wametengeneza! Ninafikiri baada ya tamko la (Freeman) Mbowe (Mwenyekiti wa CHADEMA) kuna namna.

"Anachojaribu kusema ni vitu ambavyo havina maana, suala la Katiba Mpya si la CCM, kwa sababu misingi ya utawala bora inajenga vizazi na vizazi, hivyo mjue kwamba CCM walikataa mapendekezo yetu kwa maandishi," Lema alisema.

Naye Heche alisema mazungumzo ya maridhiano yalikwama kutokana na CCM kukataa hoja zao za Katiba Mpya na kuwa na mfumo mpya wa uchaguzi. Si kutokana na viongozi wa CHADEMA kutoa lugha chafu kwenye mikutano ya hadhara alivyodai Kinana juzi.

"Sisi kama chama cha siasa, tunataka mazingira bora ya uchaguzi ili Watanzania wapate uhuru wao wa kuamua nani awe kiongozi wao, hatukwenda kwenye mazungumzo ili tubadilishe lugha za kuikosoa CCM, na wakati mwafaka chama chetu kitazungumza kuhusu mambo haya," alisema Heche.

**WADAU WALONGA**

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Ananilea Nkya, aliiambia Nipashe jana kuwa ili kupata suluhu ya mambo ambayo vyama vya upinzani wanadai, ni lazima kuzingatiwe mambo mawili ikiwamo kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi.

Alisema uchambuzi wa miswada iliyopitishwa na Bunge, umebaini hatua iliyofikiwa haiwezi kuleta mapinduzi ya kweli ambayo yatatengeneza sheria ambazo zitaleta mageuzi ya kweli kwenye masuala ya uchaguzi.

Alisema tume itakayotokana na miswada hiyo haiwezi kutibu matatizo ya uchaguzi ambayo yamekuwa chanzo cha mazungumzo kati ya CCM na CHADEMA.

"Wadau wamekuwa wakidai tume huru ya uchaguzi, lakini tume hiyo haiwezi kuja tu kwa sababu kuna sheria zimekuja bungeni kufanyiwa marekebisho. Kulihitajika marekebisho madogo ya katiba ambayo yataleta Tume Huru ya Uchaguzi," alisema.

Naye Abbas Mwalimu, Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia na Mchambuzi wa Masuala ya Siasa, alisema maridhiano si kitu cha dakika 10, bali mchakato unaohitaji muda ili kukamilisha dhima yake ya kuaminiana, kuwa na uwazi na kuonesha nia ya utekelezaji kwa pande zote juu ya yale yatakayojadiliwa.

"Katika suala la Tume Huru ya Uchaguzi, mimi nina wasiwasi kwa sababu unapohitaji serikali iajiri watumishi kwenye tume hiyo watakuwa wakifanya kazi takribani miezi mitatu tu kila baada ya miaka minne. Huo muda mwingine watakuwa wamekaa tu, sasa hapo serikali itakuwa inalipa mamilioni ya shilingi kwa mwezi bila sababu.

"Ninachoshauri kuwe na uwazi wa kutosha katika tume iliyopo. Na bado kuna nafasi pande zote zinaweza kukaa waangalie nini cha kufanya wapate suluhu ya pamoja ya kuaminiana ili mengine yaendelee na wajipe muda kutatua ambayo hayajapatiwa ufumbuzi," alishauri Mwalimu.

Mwalimu pia alitoa wito kwa CHADEMA kujitathmini, akiwa na ufafanuzi kuwa kuna haja kukaa na kutazama hoja 11 na kuona ni zipi zilizokubaliwa waende nazo na ambazo bado wajipe muda ili zipatiwe ufumbuzi.

## Posta, TTCL hoi, wabunge wataka 'zibebwe' madeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SHIRIKA la Shirika la Posta Tanzania (TPC) limeelemewa madeni kiasi cha kushindwa kujiendesha, Bunge limeazimia serikali ibebe deni lake la Sh. bilioni 26.8 ili kusafisha mizani ya shirika kuliwezesha kukopesheka.

Bunge pia limeazimia serikali ihakikishe Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL) iwezeshwa kifedha ili kuwa na mtaji wa kujiendesha kibiashara.

Ilielezwa bungeni jana kuwa TPC imeelemewa na madeni, ikishindwa kuwasilisha kodi na riba mbalimbali kwa wakati ambazo ni Kodi ya Mishahara (PAYE), Kodi ya Kuendeleza Ufundi Stadi (SDL) na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kati ya mwaka 2007 na 2016.

Changamoto nyingine inayolitikisa shirika hilo ni kuwa na mtaji hasi wa uendeshaji wa Sh. bilioni 35.2 kwa hesabu za mwaka wa fedha 2021/22.

Jana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Kakoso, alibainisha hayo bungeni jijini hapa alipowasilisha taarifa ya kamati hiyo kuhusu shughuli za kamati kwa mwaka 2023, akisema licha ya serikali kufanya jitihada kubwa kufufua shirika hilo, changamoto hizo zinakwamisha maendeleo ya shirika kibiashara.

Alisema Bunge linaitaka serikali iongeze mtaji kwa shirika hilo ili kuhakikisha linapata kamisheni kwa kila mzigo. Shirika pia libuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiendesha kibiashara.

Kuhusu TTCL kushindwa kujiendesha kibiashara, Kakoso alisema Bunge linaazimia serikali ihakikishe kampuni hiyo inawezeshwa kifedha ili iwe na mtaji wa kujiendesha kibiashara.

Alisema Bunge pia linaagiza mfumo wa sheria za ajira serikalini uangaliwe ili kuruhusu kampuni zinazojiendesha kibiashara kuwa na taratibu za ajira zinazoruhusu kuunda ushindani. Pia kampuni hiyo iongeze kasi kuunganisha wateja.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrew Kundo, alisema serikali inawekeza nguvu katika uchumi wa kidijitali.

"Uchumi huu unahitaji miundombinu ya kidijitali na miundombinu hii ni pamoja na ujenzi wa mikongo, ukianzia mkongo wa baharini, mkongo wa taifa, last mile connectivity ambao inahusisha minara pamoja na fiber mlangoni kwako," alisema Kundo.

## HABARI KITAIFA

# Hospitali Temeke yaanza huduma mume kushuhudia mke akijifungua

**Na Pilly Kigome**

HOSPITALI ya Temeke imeanza rasmi kutoa huduma ya kujifungua huku mwenza au ndugu wa karibu wakishuhudia na kuchagua muuguzi anayemtaka.

Akizungumza na Nipashe, Daktari Mfawidhi kutoka Temeke, Joseph Kimaro alisema na hatua hiyo inatokana na mwongozo mpya wa chati uchungu unavyosema.

Alisema huduma hiyo imeanza Februari 4, mwaka huu na imepokewa kwa furaha kwa baadhi ya wahitaji.

Mmoja wa mwenza aliyekwenda kujifungua hospitalini hapo jana, Hassan Mwauta, alisema alipokea kwa furaha kubwa tangazo hilo na amewiwa kumsaidia mke wake katika huduma hiyo kutokana na huruma na mapenzi aliyonayo kwa mke wake.

"Nimemleta mke wangu kuja kujifungua nilisikia kuna huduma ya mzazi kujifungua akiwa na mwenza wake hospitalini hapa, sikuamini nimejionea mwenyewe nimeshangaa kwa kweli mazingira mazuri na huduma nzuri, unaweza kuingia na mjamzito wako ukakaa naye muda wowote unaotaka," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, baadhi ya wajawazito kutoka hospitalini hapo walisema hatua hiyo ni nzuri kwa mabinti wadogo wanaopata mimba za utotoni itawawezesha kurahisisha binti kuwa na msaidizi katika hali hiyo ya kujifungua.

Hata hivyo, mwanamke mmoja aliyekuwa anasubiri kujifungua, alibeza hatua hiyo akisema inaweza kuwafanya wajawazito wabweteke wakati wa kujifungua kwa kuamini kuwa ndugu yake atamsaidia katika hali hiyo.

Ofisa Mkunga wa hospitali hiyo, Shukrani William, alifafanua kuwa hospitali iko tayari na imejiandaa kwa kiwango kikubwa kutoa huduma hiyo kwa wananchi kwa kuwa wodi ya kujifungulia imeboreshwa kwa kiwango kikubwa, ili kumwezesha mjamzito kupata huduma bora zaidi na kuwa karibu na msaidizi wake pamoja na kuzingatia utu na heshima.

Maboresho hayo ni moja ya mikakati ya kuunga mkono jitihada za serikali kuona sekta ya afya inaboresha huduma zake na maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Hospitali ya Rufani kimkoa wa Temeke inaendelea kufanya maboresho ya kimiundombinu ili iweze kutoa huduma bora zaidi kwa Watanzania.

Hatua hiyo ni juhudi za kupunguza ama kuondoa vifo vitokanavyo na uzazi nchini kwa kuleta ukaribu na usaidizi katika hatua hiyo.

Mei 2023 Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Angellah Kairuki, alibainisha sababu kubwa za vifo hivyo ni inayohusu mfumo wa afya ikiwamo upatikanaji mdogo wa huduma bora za afya, uhaba wa wahudumu afya wenye ujuzi, mifumo dhaifu ya rufani, vifaa tiba, dawa za vitendanishi na uratibu duni kati ya sekta za umma na binafsi.

Katika sababu za nje ya mfumo wa afya ikiwamo ushiriki duni wa jamii na ushirikishwaji katika kupanga uzazi utekelezaji, baadhi ya imani potovu, mila na desturi za kitamaduni na ile ukosefu wa usawa wa kijinsia. Katika juhudi ya kupunguza vifo hivyo vitokanavyo na uzazi takwimu kutoka Wizara ya Afya inasema vifo vimepungua kutoka vifo 530 kwa mwaka 2015/16 na kupungua kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

Hatua hiyo imepunguza vifo kwa asilimia 80 nchini kwa mujibu wa ripoti ya utafiti ya afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria ya mwaka 2022.

# Aliyenunuliwa cherehani, ataka kumshonea Rais Samia nguo

**Na Halfani Chusi**

UTHUBUTU unalipa, ndivyo unavyoweza kusema! Baada ya mbunifu na mshonaji, Beatrice Mwalingo, aliyeomba zawadi ya cherehani kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia ukurasa wa Instagram, kuthibitisha kupokea nne.

Beatrice alitoa ombi hilo wakati Rais Samia akiwa safarini nchini Indonesia kwa ziara ya siku tatu ya kikazi Januari 24, mwaka huu.

Beatrice aliweka ujumbe wake kwa kumwomba Rais Samia akirejea kutoka Indonesia amletee zawadi ya cherehani na muda mchache baadaye Rais alimjibu kwamba amepata wasaha wa kusoma ujumbe wake na kumwahidi kuwa wasaidizi wake watawasiliana naye.

Akizungumza kwa furaha kupitia ukurasa wake, Beatrice alisema haamini kama ombi lake limejibiwa na hakutegemea kama angepata cherehani nne.

"Leo ninayo furaha kubwa sana, kuwaambia kama huwezi amini cherehani nilizoomba hizi hapa, zimekuja hizi hapa nne, siyo moja, nne eeeh, jamani hivi mnafikiri ninaweza kulala kweli mimi, aaah silali!" alisema Beatrice.

Alisema amefurahi kwa kuwa hakutarajia alivyojibiwa alihisi atapata moja na kumshukuru Rais kwa kumwagizia zaidi ya moja na kwamba hatua hiyo imemvusha.

"Nimeletewa nne, mbili za kudarizi na mbili za kushona kawaida kwa sasa ninakuwa na jumla ya cherehani 14, ule muda ambao nilikuwa naenda kuazima kwa wengine sasa sitaupoteza tena," alisema Beatrice ambaye pia anajishughulisha na ufugaji wa kuku na bata.

Alisema wakati anaanza kazi hiyo alikuwa na vijana 12 ambao kwa sasa wengine wamesafiri na amebaki na saba na anatarajia kuongeza wafanyakazi wengine wanne kutokana na ongezeko hilo.

"Ninamshukuru sana Rais kwa kitu alichonifanyia, sikuwahi kufikiria wala kuwaza alivyonijibu kwamba atanipatia, imenifungulia milango kwenye mambo mengi sana, vijana wengine wamekuja kujifunza kwa sababu walikuwa wanazichukulia kazi za ufundi kama za wazee," alisema.

"Tuitumie mitandao kuwasilisha shida zetu, hata kama unayemlenga hatakusaidia, anaweza akaona mtu mwingine akaguswa, lakini kwa sasa ninatamani kumshonea Rais nguo, kama nitapata nafasi nimpime mwenyewe nichukue vipimo kwa ufasaha.

"Wakati ninasubiria ombi la kwenda kumpima, ninataka nimpe zawadi ya kuku kupitia wasaidizi wake, maana mimi pia ninajishughulisha na ufugaji, ninafuga bata na kuku wa kienyeji kwa leo ninaomba wamfikishie jogoo watano iwe zawadi yangu ya birthday kwake," alisema Beatrice.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UPEMBUZI YAKINIFU KUHUSU KUBORESHA UPATIKANAJI WA MAJI KWA JAMII, KWA AJILI YA MIFUGO, MATUMIZI YA NYUMBANI NA KUNYWA.**
**KUMBUKUMBU NA: REQ-00000450**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD) inaalika kampuni au taasisi zenye uzoefu na sifa nzuri kuonyesha nia yao ya kufanya Upembuzi yakinifu kuhusu Upatikanaji wa huduma za Maji kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Kampuni ya EACOP inajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (hapa ikijulikana kama "Mradi") unahitaji Ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Bomba pamoja na miundombinu mingine. Baadhi ya jamii zilizo kando ya ukanda wa bomba zinakabiliwa na changamoto (zisizohusiana na EACOP) za upatikanaji wa maji ya kunywa, maji kwa matumizi ya nyumbani na maji ya mifugo.

EACOP inapanga kufanya upembuzi yakinifu wa kutambua hatua za msaada wa hiari kwa baadhi ya jamii hizo. Hatua hizo zinaweza kujumuisha ukarabati wa visima vya jamii au vyanzo vingine vya maji, kuchimba visima vipya katika maeneo ambayo hakuna visima vinavyofanya kazi, ukaguzi wa mabwawa ya sasa na hali yao ya utendaji, na ukarabati au ujenzi wa mabwawa mapya. Upembuzi yakinifu utajumuisha upitiaji wa taarifa zilizopo na kiasi kidogo cha kazi kitafanyika kwenye maeneo ya mradi.

Ili kufanya upembuzi yakinifu, EACOP inahitaji shirika (shirika binafsi au lisilo la kiserikali) lenye rekodi ya uzoefu wa kutoa huduma ya maji kwa jamii za vijijini nchini Tanzania, hasa katika mikoa ambayo EACOP itapita, (EACOP inavuka mikoa nane (8), ikiwa ni pamoja na Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga na kufunika halmashauri ya wilaya 27, na vijiji 231), ikiwa ni pamoja na kuonyesha;

- Uzoefu katika kufanya upembuzi yakinifu kuhusu upatikanaji wa maji, hasa juu ya:
  - Kuandika Ramani ya Upatikanaji wa Maji ya Ardhi, Maji ya Juu, na Maji ya Mvua.
  - Tathmini ya utendaji na matengenezo / ukarabati wa vyanzo vya maji vilivyopo
  - Hidrojiolojia
  - Kutathmini uwezo wa kamati za usimamizi wa maji na miundo ya serikali ya utawala wa maji
  - Mazingira ya taasisi na mahitaji ya idhini
- Uzoefu wa ziada katika utekelezaji wa ufumbuzi wa kuboresha upatikanaji wa maji kwa jamii. Shirika linapaswa kuonyesha kuwa limeanzisha uhusiano na wadau muhimu wa sekta ya maji nchini Tanzania.
- Ushahidi wa uwezo wao wa kufanya kazi hiyo na timu yenye sifa na uzoefu.

**VIGEZO MUHIMU:**
Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, ujuzi kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA).
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana ikiwa ipo.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ametuma maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Kampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **20/02/2023**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **REQ-00000450 Utoaji was huduma ya maji.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni zilizoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya kampuni zenye vigezo. Mwaliko kwa kampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni za Awali zenye vigezo baada ya kampuni hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.



Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga (kushoto), wakitia saini mikataba ya maji na makandarasi kutoka Kampuni ya Geo Spatia Classic Work LTD, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji wilayani Kishapu jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Foleni meli za mafuta Bandari Dar zapigiwa kelele bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam inakabiliwa na changamoto ya kasi ndogo ya ushushaji wa shehena na kusababisha msongamano mkubwa, ikiwamo meli za mafuta zilizoko kwenye boya la kuhudumia mafuta ghafi (SPM) kwa kutumia wastani wa siku 10.

Aidha, Bunge limeambiwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), inakosa udhibiti wa mapato yanayotokana na tozo za huduma ya matumizi ya gati zake ambayo yangewezesha maboresho ya miundombinu.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeazimia serikali ijenge gati mbili za dharura (kwenye gati 0) katika Bandari ya Dar es Salaam, ambazo zitakuwa na uwezo wa kubeba mzigo mkubwa uliopo bandarini.

Akiwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa mwaka 2023, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Kakoso, alisema Bunge linaazimia TPA iongeze kasi ya kuboresha miundombinu ya barabara na njia ya reli inayoingia na kutoka Bandari ya Dar es Salaam.

Kuhusu Mamlaka ya Bandari Tanzania, kutobakiziwa sehemu ya fedha inazokusanya kutokana na tozo za gati, Bunge linaazimia kwamba, serikali iwape TPA Sh. bilioni 35 kila mwezi, kutoka kwenye makusanyo ya matumizi ya huduma za gati.

"Kwa kuwa, taarifa zilizowasilishwa kwenye kamati zinaonyesha kwamba, mapato yanayokusanywa na TPA kutokana na tozo za gati yanachukuliwa na serikali bila TPA kubakiziwa kiasi chochote.

...Na kwa kuwa, utaratibu huo unaminya uwezo wa TPA kufanya maboresho ya miundombinu katika magati hayo, jambo hilo linaweza kupunguza ufanisi wa huduma za bandari katika magati hayo na kuipunguzia serikali uwezekano wa kupata mapato zaidi kutokana na huduma za bandari.

"Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, serikali iwape TPA kiasi cha Sh. bilioni 35 kwa kila mwezi kutoka kwenye makusanyo ya wharfage."

**MADENI**

Kuhusu changamoto za sekta ya ujenzi, hasa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Mfuko wa Barabara (RFB), alisema wakala huyo anakabiliwa na changamoto ya kupungua bajeti ya miradi ya maendeleo na matengenezo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti, mpaka Desemba 2023, fedha za ukarabati/matengenezo ilizopokea ni Sh. bilioni 369 na kutokana na mvua inayoendelea kunyesha hazitoshelezi.

Aidha, ucheleweshaji wa kulipa madeni ya makandarasi na wahandisi washauri kwa wakati kwenye miradi na kusababisha kuongezeka kwa gharama hadi Desemba, mwaka jana.

"Miradi iliyokamilika ni 94, na makandarasi wanadai Sh. bilioni 386.36. Pia, miradi ya barabara inayoendelea ni 69, deni la makandarasi ni Sh. bilioni 392.608.

...Hivyo jumla ya deni lote la makandarasi mpaka kipindi hicho, ni Sh. bilioni 778, na linaweza kuongezeka kwa utaratibu wa riba katika miradi."

Kamati hiyo, imesema pia TANROADS inakabiliwa na tatizo la kuchelewa kwa tathmini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi inayosababishwa na sheria ya fidia.

Kakoso ambaye ni Mbunge wa Mpanda Vijijini (CCM), amefafanua kuwa, hadi Desemba 2023, fidia inayohitajika kwenye maeneo yote nchini, kwa barabara kuu na za mikoa, inakadiriwa kufikia zaidi ya Sh. trilioni 5,588.

Akichangia mjadala wa taarifa hiyo, Mbunge wa Same Mashariki (CCM), Anne Kilango, alisema TANROADS, ina barabara 71 nchini zenye urefu wa kilomita 2,000 zilizopaswa kutengenezwa mwaka 2023/24.

Alisema barabara hizo ambazo zimeisha muda wake, zinahitaji Sh. trilioni 3.26 ili kuzihuisha upya.

Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, wakati anachangia hoja ya TPA, alisema ni lazima kuwe na uwekezaji wa kutosha, kwa kuwa hata eneo la kuhifadhia mafuta ni dogo. Hivyo, ni lazima serikali ione namna ya kuongeza fedha kusaidia miradi hii.

Naye Innocent Kalogeresi, Morogoro Kusini (CCM), alisema TANROADS inaweza kufanya mambo makubwa nchini tatizo ni fedha.

**MBARAWA AJIBU**

Akijibu hoja za wabunge kuhusu maeneo hayo, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema ongezeko kubwa la meli katika Bandari ya Dar es Salaam, ni baraka kubwa kwa nchi na imeleta changamoto kubwa ya kujipanga kuzitatua ili isiweze kujitokeza tena.

Waziri Mbarawa alisema katika kutekeleza mpango huo, serikali imeamua kujenga gati kubwa, lenye urefu wa mita 590 katika eneo la Malindi, ambalo litakuwa na uwezo wa kuwekeza meli mbili kwa wakati mmoja.

"Hivi ninavyozungumza tunatafuta mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo, na pesa ipo kwa ajili ya kazi hiyo," alisema.

Aliutaja mkakati wa pili, ni kujenga bandari ya kisasa, kwa ajili ya ushushaji wa mafuta pamoja na matangi ya kuhifadhia mafuta.

Alisema mradi huo unaendelea na hadi sasa mkandarasi amepatikana kwa ajili ya kazi hiyo, huku kiasi cha Sh. bilioni 560 kikitarajiwa kutumika kwa kazi hiyo.

"Hatua ya pili itakayofuata ni kujenga bandari hiyo Bagamoyo kwa ajili ya kuteremshia mafuta ili kupunguza msongamano wa meli za mafuta ambao upo kwa sasa."

Alisema hatua ya tatu ambayo wanaendelea nayo kupunguza msongamano ni kuendelea kujenga bandari, gati namba 13 mpaka 15, na kwamba wapo katika hatua za kupitia dizaini ya mradi huo ili kuitangaza na apatikane mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo.

---

MARADHI YA FIGO

## Makonda ashangaa mkoa hauna huduma ya usafishaji damu

**Na Beatrice Shayo,** KATAVI

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ameshangaa kukosekana jengo la matibabu ya kusafisha damu wagonjwa wa figo mkoani Katavi licha ya serikali kutoa vifaa kwa ajili ya huduma hiyo.

Ameagiza kutafutwa Sh. milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo kutoka kwenye mapato yao ya ndani badala ya kusubiri serikali kuu ili kuokoa maisha ya wananchi.

Makonda aliagiza hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Mpanda ambao walilalamikia kufuata huduma ya kusafisha damu mkoani Mbeya, hivyo kutumia gharama kubwa kupata matibabu.

"Mbona wakija viongozi wanatafuta fedha wanachanga, ina maana ukipita Mwenge wa Uhuru hamchangi? Kwanini hilo jengo halikamiliki wakati tayari vifaa vimeshaletwa? Mnahatarisha afya za wananchi.

"Mtu akifanyiwa huduma ya kusafisha damu anatakiwa kupumzika ina maana anaingia gharama za kwenda kumweka hoteli ili kusubiri anapokuwa vizuri arudi nyumbani kwake Katavi. Kama hana hiyo fedha unahatarisha afya yake," alisema.

Makonda aliwaagiza viongozi wa mkoa kuhakikisha wanamtafuta Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kuwa anaamini atawasaidia ili kuokoa afya za wananchi hao wanyonge ambao wanatumia gharama kubwa kwenda kupata matibabu ya figo mkoani Mbeya.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Mkoa wa Katavi, Dk. Joseph Mkandi, alisema serikali imejitahidi kwenye ujenzi na ukarabati wa hospitali hiyo mpya, lakini ina majengo ambayo hayajakamilika ikiwamo jengo la kuweka mashine hiyo na wameomba waongezwe fedha.

Baada ya kutoa maelezo hayo, Makonda alihoji mashine hiyo ilikohifadhiwa. Dk. Mkandi alisema kuna miundombinu ambayo inatakiwa kuwekwa ili vifaa hivyo viweze kufanya kazi, hivyo wamehifadhi sehemu salama kusubiri kukamilika kwa jengo hilo ili waanze kutoa huduma.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Kaster Ngonyani, alisema ndani ya miezi minne wamefanikiwa kutokomeza kundi la uporaji mitaani, maarufu 'Damu Chafu'.

Alisema vijana hao wana umri wa kati ya miaka 18 na 24. Jeshi la Polisi limewakamata zaidi ya vijana 60 waliobainika kuhusika katika matukio ya uhalifu na kuchukuliwa hatua.

## HABARI KITAIFA

# NEMC yataka halmashauri zitumie taka kama fursa

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeyataka majiji na manispaa kuweka mikakati ya kuzigeuza taka ngumu kuwa fursa ya ajira na kuzitumia kutengenezea nishati na bidhaa mbalimbali kama sehemu ya kuyaweka maeneo yao katika hali ya usafi.

Jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Semesi, alitoa rai hiyo wakati akifungua mkutano ulioandaliwa na Kituo cha Sayansi ya Mazingira (CSE) cha India kuhusu udhibiti wa taka ngumu.

Mkutano huo uliwashirikisha maofisa kutoka manispaa na majiji kwenye mikoa mbalimbali nchini, lengo likiwa kujenga uelewa na mikakati ya kusimamia mazingira kwenye eneo la taka ngumu.

Alisema ni umuhimu kukusanya takwimu za taka zinazozalishwa kwenye maeneo mbalimbali nchini na namna zinavyotunzwa ili ziwe fursa kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali, hali ambayo itasaidia kuweka mazingira katika hali ya usafi.

Alisema taka ngumu zinaweza kutumika kuzalisha nishati na kuwakomboa wananchi wengi kiuchumi na kuongeza kuwa kituo cha CSE cha India tayari kimetengeneza mwongozo wa namna ya kuzitumia taka hizo kama rasilimali.

"Taka ngumu kwenye manispaa zetu Tanzania zinaendelea kuongezeka kutokana na wingi wa watu na shughuli za binadamu, hivyo tunapaswa kuangalia namna ya kutumia taka ngumu kama fursa na tukifanikiwa kwenye hili tutayaweka mazingira yetu safi," alisema.

Alibainisha kuwa takwimu ambazo si rasmi, zinaonesha Mkoa wa Dar es Salaam pekee unazalisha tani 400,000 za taka wakati nchi nzima inakadiriwa kuzalisha tani milioni 12,000 za taka kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Utafiti wa Mazingira (NEMC), Dk. Menan Jangu, alisema kuna haja ya kuboresha mifumo ya udhibiti wa taka ngumu ambazo zimekuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira nchini.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali. Kwa kushirikiana na CSE wanaweka mikakati ya kuhakikisha taka ngumu zinakuwa fursa.

Alisema kwa kushirikiana na CSE wamefanya mambo mengi kwenye usafi wa Ziwa Victoria ambalo awali lilionekana kuwa hatarini kutokana na ongezeko la uchafuzi unaotokana na taka ngumu.

"Tatizo letu kwa sasa hatuna takwimu sahihi kuonesha kwenye maeneo yetu tunazalisha taka kiasi gani, za aina gani na zinakwenda wapi, lakini ushirikiano na kituo cha CSE tumejitahidi kufanya kazi kupunguza tatizo hili," alisema.

# Wananchi wakosa maswali ya kumuuliza mbunge wao

**Na Munir Shemweta,**
MLELE

WANANCHI wa Mwamapuli, Jimbo la Kavuu, Halmashauri ya Mpimbwe, mkoani Katavi wamekosa maswali ya kumuuliza mbunge wao ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, kutokana na kutekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizozitoa wakati wa kampeni ya uchaguzi mwaka 2020.

"Hivi mna kero hapa kweli? Kuna mtu ana jambo la kumwuliza mbunge kuhusu alichokuwa anasema wakati wa kampeni? Na kama yupo anyanyue mkono na aseme," alihoji Pinda.

Hayo yalijitokeza juzi wakati mbunge huyo akiwafariji wananchi waliopatwa na ugonjwa wa kipindupindu katika eneo la Mwamapuli Halmashauri ya Mpimbwe, mkoani Katavi.

Akiwa katika eneo hilo, Pinda aliwataka wananchi wa Mwamapuli kufanya kazi kwa bidii na kuweka wazi kuwa inapoelezwa kuwa eneo la Mwamapuli lina changamoto anahakikisha ameifanya kazi.



"Wana Mwamapuli, ukisema kuna changamoto ninaitafutia ufumbuzi usiku na mchana. Tulikuwa na changamoto nzito lakini tumeziamua na zimebaki za kawaida tu," alisema.

Pinda aliwaomba wananchi wa jimbo hilo kutorudi nyuma katika kufanya kazi na kuwaeleza kuwa Jimbo la Kavuu "liko juu" hususan katika uzalishaji mazao kama vile mahindi na mpunga huku akiwaeleza wananchi wa jimbo hilo kuisikia kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan ya 'Kazi Iendelee'.

Akizungumzia ugonjwa wa kipindupindu uliowakumba baadhi ya wananchi wa Mwamapuli, Pinda aliwataka wananchi wa eneo hilo kuanza juhudi za kutokomeza ugonjwa huo kwa kuwa wasafi pamoja na kuhakikisha kila nyumba inakuwa na choo.

"Ninataka ugonjwa huu uondoke kwa siku moja kwa kuhakikisha mnakuwa safi na mnachemsha maji, mnaniahidi kuondoa kipindupindu ndani ya siku moja?" alihoji.

Naibu Waziri Pinda alikuwa jimboni kwake kwa ziara ya siku moja ambapo alifanya shughuli mbalimbali kama vile ukaguzi wa barabara ya kilomita 70 ya Kibaoni - Sitalike, kukabidhi magari ya wagonjwa pamoja na kuwafariji wananchi waliopatwa na ugonjwa wa kipindupindu kwenye eneo la Mwamapuli.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: MAENDELEO NA MAFUNZO KUHUSU USALAMA NA UONEKANO BAHARINI, RASI YA CHONGOLEANI. KUMBUKUMBU NA: REQ-00000466**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD) inaalika makampuni au taasisi zenye uzoefu na sifa nzuri kuonyesha nia ya kutekeleza ubunifu na utoaji wa programu kwa wavuvi kwenye Rasi ya Chongoleani iliyopo mkoa wa Tanga, Tanzania kwa mafunzo na msaada ili kuboresha usalama na uonekano baharini kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirishwa kwenye masoko ya kimataifa Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchi ya Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Kwa Tanzania, Bomba la mafuta linapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (hapa ikijulikana kama "Mradi") umeanza ujenzi wa kituo cha kuhifadhia mafuta Baharini, Gati ya Kilomita 2 Baharini na kituo cha kujaza Mafuta ambapo Meli zinaweza kufungwa salama. Shughuli za jamii Baharini hususani uvuvi na uokotaji zitakumbwa na athari wakati wa ujenzi na uendeshaji wa Gati ambapo maeneo yaliyozuiliwa yataimarishwa.

Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki unatafuta kufanya makubaliano na shirika linalojikita katika usalama wa baharini na mafunzo ili kuendeleza na kutoa mafunzo kwa wanajamii husika kulingana na kipengele cha usalama na uonekano baharini chini ya programu ya urejeshaji wa hali ya maisha (kipato) cha waguswa wa Bomba la Mafuta. Shirika linatakiwa liwe na sifa na vigezo vifuatavyo:

- Uzoefu katika kuendeleza na kutoa mafunzo kwa jamii kuhusu usalama baharini kwa watumiaji wa bahari ambao huenda hawajui kusoma. Hii itahitaji vifaa vya mafunzo vinavyotegemea vitendea kazi vya kuona, alama au maelekezo ya vitendo badala ya maelekezo ya maandishi au mazungumzo.
- Uelewa wa kushughulikia na kusimamia vyombo vya wavuvi wadowadogo, usafirishaji na kutia nanga. Ufahamu wa changamoto na hatari maalum baharini ikiwa ni pamoja na mienendo ya hali ya hewa, mawimbi, uwezekano mkubwa wa hatari na taratibu pindi dharura zinapotokea.
- Uzoefu wa kutoa vifaa vya msingi vya usalama kwa wavuvi wadogowadogo.
- Uzoefu wa kuanzisha mifumo rahisi ya mawasiliano ya baharini yanayofaa kwa wavuvi wadogowadogo kwa kushirikiana na wanajamii wanaotumia bahari na mamlaka husika kwenye mifumo rahisi ya usajili na utambulisho wa vyombo vya baharini.

**VIGEZO MUHIMU:**
Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:

- Maelezo ya miradi inayofanana na hii au shughuli zilizofanywa hapo awali, ambazo zinatoa ushahidi wa timu iliyofuzu na ipo tayari, uzoefu wa kufanya kazi na wanajamii na rekodi ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka husika za Usajili nchini Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA).
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana ikiwa inafaa.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Kanzidata ya watoa huduma wazawa (LSSP) ya EWURA au uthibitisho wa maombi ya kusajiliwa kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia, hili linasisitizwa sana.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani ya Nchi za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za kifedha za kampuni kwa mwaka husika.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE) na mchakato wa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi inayofanana.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **20/2/2024.** Kichwa cha Barua Pepe kiwe: REQ-00000466 Mafunzo kuhusu usalama baharini. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itakagua na kutathmini nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa makampuni husika.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *RC Malima ameonesha mfano apewe ushirikiano*

**TATIZO** la uhaba wa sukari na kupanda bei kwa bidhaa hiyo kumeathiri watu wengi hasa wenye kipato cha chini.

Baadhi ya maduka ya bidhaa hiyo inauzwa mpaka Sh. 5,000 kwa kilo moja na wengine kutoipata madukani.

Pamoja na serikali kutoa bei elekezi, lakini baadhi ya wafanyabiashara wanadai bei wanayonunulia ni kubwa hivyo ili wapate faida lazima nao wauze kwa bei kubwa.

Wafanyabiashara wengine wanaficha bidhaa hiyo ili ikosekane kwenye soko na wapate fursa ya kulangua kwa bei kubwa na kupata faida maradufu.

Katika kukomesha hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, ameamua kutoa namba yake ya simu ya kiganjani kwa wananchi wa mkoa huo ili wampigie simu au kutuma ujumbe mfupi wanapouziwa sukari kwa bei ya juu tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,700 hadi 3,200 na wafanyabiashara ili waweze kukamatwa na kuchukulia za kisheria.

Licha ya Mkoa wa Morogoro kuwa na viwanda vinne vya sukari kikiwamo cha Mtibwa, Kilombero I na II pamoja na kiwanda kipya cha Mkulazi, kuna tatizo la upungufu wa bidhaa hiyo nchini na serikali kulazimika kuagiza tani 100,000 kutoka nje.

Awamu ya kwanza ya shehena ya sukari kutoka nje imeshawasili na bei elekezi ya kuuzwa imewekwa kwa kilo ni Sh. 2,700 mpaka 3,200 kulingana na maeneo ambayo ipo kisheria na wafanyabiashara wanapaswa kuuza kwa kuzingatia bei hizo.

Hata hivyo, imeelezwa kuwa upungufu uliojitokeza wa bidhaa hiyo umechangiwa na viwanda kushindwa kuvuna miwa kutokana na mashamba kujaa maji kwasababu ya mvua za mafuriko na kusababisha uvunaji wa miwa na kupelekwa viwandani kukwama.

Asilimia 70 ya sukari yote nchini inazalishwa katika Mkoa wa Morogoro na hali hiyo ya mvua imesababisha miezi mitatu iliyopita kutokuwa na uzalishaji kutokana na mashamba kujaa maji.

Malima ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Morogoro, alifanya jukumu la kuzunguka maeneo ya mashamba hayo kila siku na kujionea Kiwanda cha Kilombero I na II, Mtibwa na Mkulazi yakiwa yamezingirwa na maji hali inayosababisha kukosekana mashine wala treka inayoingia kwenye mashamba hayo.

Uamuzi aliouchukua Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wa kutoa namba yake ya simu unapaswa pia kuchukuliwa na viongozi wengine, ili watu wanaopandisha bei ya bidhaa hiyo kiholela waripotiwe na kuchukuliwa hatua.

Kuwaficha walanguzi na kuwaacha wakiwaumiza watu kwa kuwauzia bei ya juu ni kuwaendekeza.

Kuanzia mwezi Novemba, Desemba, Januari na Februari zaidi ya tani 70,000 zilizopaswa kuzalishwa zimeshindikana kutokana na mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya mkoa huo ambao una viwanda vingi vinavyotegemewa.


Hata hivyo, kuingia kwa meli tatu zenye kontena za bidhaa hiyo kunaleta tumaini la kushuka kwa makali ya bei hasa ikizingatiwa wiki chache zijazo waamini wa dini ya kikristo na kiislamu wataanza kufunga Kwaresima na Ramadhani.

Kipindi hicho cha mfungo ndicho watu wanatakiwa kutubu dhambi zao na wafanyabiashara pia wanatakiwa kuuza bidhaa kwa bei halali kama sehemu ya ibada yao.

Wafanyabiashara wasitumie kipindi hicho kuwaumiza watu wanaotimiza wajibu wao kwa Mungu kwa kuwa wanajua lazima watanunua.

Wananchi wameomba pia wakuu wa wilaya zote kutoka ofisini na kwenda kufanya msako kwa wafanyabiashara wanauza sukari kwa bei ya juu tofauti na bei elekezi ya maelekezo ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# *TARURA ijenge madaraja kunusuru wanafunzi*

**WANAFUNZI** wa shule za msingi na sekondari wanakumbana na matatizo mengi kuifikia elimu, mosi wanatembea kilometa nyingi kufika shuleni, hawana mabweni na chakula na wengine wakipata mimba hata kuozwa utotoni.

Kama hiyo haitoshi, ipo shida nyingine inayohatarisha maisha yao, ni miundombinu mibovu ya madaraja na barabara wakati wa mvua.

Mbali na kuwakwamisha kielimu inaweza kusababisha vifo nyakati za mafuriko hasa wakati huu wa mvua za el nino.

Wanafunzi huvuka madaraja kwenda shuleni na kurudi nyumbani, hupita mabondeni na kwenye barabara zilizo juu ya mikondo ya maji au mito. Huko hukutana na madaraja ya miti na kamba ambayo si salama kwao hasa kama kuna mamba walio ndani ya mto.

Katika maeneo mengine, wanafunzi huvuka mito kwa kutumia mitumbwi na hutokea kipindi wanajazana kupita kiasi jambo ambalo pia ni hatari kwao.

Itoshe kusema ni bora kukinga kuliko kuponya, wakati umefika Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuboresha miundombinu hiyo sehemu zote kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na watu wengine pia.

Inasikitisha kuona video zinazorushwa katika mitandao ya kijamii zikionyesha jinsi wanafunzi wanavyohangaika kuvuka mito yenye maji kutokana na ukosefu madaraja, TARURA na mainjinia wa barabara kwenye halmashauri mko wapi?

Kama ni maeneo ambayo yanatakiwa kuwekea vyombo vya usafiri, basi viwekwe, na kama kujenga madaraja, yajengwe maana ni jukumu lenu na pia ni haki ya Watanzania kulindwa maisha na uhai wao.

Kwa kujenga madaraja hayo na kuhakikisha ulinzi wa mito mikubwa kwa midogo hasa kuzingatia kuacha shughuli za binadamu kama kilimo na kuchota mchanga kwa umbali wa mita 60 mto mkubwa na 30 kwa midogo wanafunzi watakuwa salama.

Watoto hawa watakuwa wamekingwa na athari hizo wakati wote wa mvua na kiangazi, hivyo TARURA wangelichukulia kwa uzito tatizo la ukosefu wa madaraja au wale wanaohusika usafiri wa majini nao waweke usalama kwenye safari zao.

Kwa sasa ni kila mahali karibu nchi mzima kuna tatizo la ukosefu wa miundombinu hiyo hali inayotishia maisha ya wanafunzi.

Kwa mfano, mwanzoni mwa mwaka jana, wanafunzi wanne walifariki dunia wakati wakivuka mto Luiche uliopo Kata ya Kagera Manispaa Kigoma Ujiji wakielekea shuleni.

Wakati hao walifariki, taarifa nyingine zilieleza kuwa mwaka huo wanafunzi zaidi 200 wa Shule ya Sekondari Simiyu iliyopo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, walikuwa katika hatari ya kusombwa na maji.

Sababu kubwa iliyoelezwa ni ukosefu wa madaraja katika mito ya Senani na Ndoba ambayo ni lazima waivuke ili kufika shuleni kwao, TARURA wanalifahamu hilo ndilo maana kuna ofisi ya Injia wa Wilaya ya Bariadi.

Hilo ni eneo moja, lakini kama ilivyoelezwa, karibu nchi nzima kuna tatizo hilo ambalo ni vyema likafanyiwa kazi mapema kadri inavyowezekana.

Mabadiliko ya tabianchi nayo yamekuwa na changamoto zake, mvua inanyesha inasomba madaraja, hivyo ni wakati wa kujipanga kukabiliana nayo kwa kuwa na miundombinu imara.

Bila kuwapo kwa hatua hizo za kuimarisha miundombinu, tunaweza kuendelea kushuhudia wanafunzi wakiteseka na kuhatarisha maisha.

Ninaamini miundombinu hiyo ikiboreshwa, wanafunzi watasoma kwa utulivu na amani bila kuhofia kwamba watarudije nyumbani.

Lakini pia utoro unaweza kupungua, kutokana na kwamba baadhi ya wanafunzi hushindwa kwenda shule kutokana na changamoto hiyo wakihifia usalama wao.

Serikali imejitahidi kujenga shule nyingi katika maeneo mbalimbali, juhudi hizo zinaweza kufifishwa na ukosefu wa miundombinu ya madaraja kwenye baadhi ya mito. Hivyo, hatua za kuwapo mazingira rafiki kwa wanafunzi kwenda shule na kurudi salama zingechukuliwa.

TANGAZO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### BEI MPYA ZA STEMPU ZA KODI ZA KIELEKTRONIKI (ETS)

**Dar es Salaam, 5 Februari, 2024:**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (2) ya Kanuni za stempu za kodi za kielektroniki za mwaka 2018, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) anapenda kuwatangazia bei mpya za stempu hizo kufuatia majadiliano yenye mafanikio makubwa kati ya Mamlaka ya Mapatao Tanzania (TRA), Umoja wa wenye viwanda Nchini Tanzania (CTI) na mkandarasi SICPA SA. Watengenezaji, Wazalishaji na Waagizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa na ambazo zimeorodheshwa katika jedwali la kwanza la kanuni za kodi za kielektroniki za mwaka 2018 watanunua stempu hizo kutoka kwa muuzaji aliyeingia mkataba na TRA kwa bei zilizoorodheshwa hapo chini.

Bei hizi mpya zimeanza kutumika kuanzia tarehe **24 Januari, 2024**. Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi ya TRA iliyopo karibu nawe au tembelea tovuti ya TRA **www.tra.go.tz** au piga simu bure kwenda namba **0800-780078** au **0800-750075** au **0800-110016,** WhatsApp **0744-233 333** au Barua pepe **services@tra.go.tz.**

| Na. | Aina ya Bidhaa | Chanzo | Bei ya zamani kwa '1000' | Bei Mpya kwa '1000' |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pombe kali, na pombe kali za mvuke | zote | 42,214.37 | 33,392.00 |
| | Mvinyo wa zabibu n.k | zote | 42,214.37 | 33,392.00 |
| 2 | Mvinyo wa matunda kama vile ndizi na nyanya n.k | Wenye matunda ya ndani kwa asilimia 75% au zaidi | 17,435.37 | 11,482.00 |
| | Sigara au bidhaa mbadala wa tumbaku | zote | 42,214.37 | 29,854.00 |
| 3 | Bidhaa nyingine za tumbaku n.k | zote | 42,214.37 | 29,854.00 |
| | Bia n.k | Zinazozalishwa nchini | 18,312.91 | 14,857.00 |
| 4 | Bia iliyotengenezwa kwa kimea n.k | Zinazoingizwa kutoka nje | 23,093.20 | 17,795.00 |
| | Juisi za matunda na mbogamboga | Zinazozalishwa nchini (kwa matunda ya ndani) | 8,082.62 | 6,889.00 |
| 5 | Juisi ya matunda ikiwemo ya zabibu, juisi ya mbogamboga zisizowekwa chachu. | Zinazoingizwa kutoka nje | 15,264.51 | 10,068.00 |
| 6 | Maji ya chupa | zote | 8,082.62 | 6,889.00 |
| | Vinywaji laini au maji yaliyoongezwa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujumuisha juisi za matunda. | Zilizo chini ya Tariff namba. 2202.10.00 | 8,082.62 | 6,889.00 |
| 7 | Vinywaji laini au maji yaliyoongezwa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujumuisha juisi za matunda. | Vinywaji vingine chini ya tariff namba 2202.91.00 na 2202.99.00 | 15,264.81 | 10,068.00 |
| 8 | Bidhaa za filamu na muziki (Yaani CD/VCDs/dvd/kanda zilizorekodiwa | zote | 16,165.24 | 16,165.24 |

Imetolewa na;

A.J.Kidata

**Kamishna Mkuu**

# Ndege maalum kutumika kusambaza dawa vituoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imesema serikali iko kwenye hatua ya kuingiza vituo vyote ya afya kuanzia zahanati hadi ngazi ya kitaifa kwenye mfumo wa kusambaza dawa kwa kutumia ndege maalum (drones) kwa ajili ya kuufanyia majaribio.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, aliyetaka kujua ni lini serikali itatumia drones kusambaza dawa katika zahanati za vijijini.

Dk. Mollel akijibu swali hilo alisema mfumo huo utasaidia kupata taarifa za kijiografia za vituo vyote nchini.

"Sasa tupo kwenye hatua ya kuingiza vituo vyote kwenye mfumo huu ili kuufanyia majaribio na pia kutazama gharama za usafirishaji dawa kupitia mfumo huo wa ndege maalum (drones) kulinganisha na usafirishaji kwa njia ya magari ili uamuzi sahihi ufanyike," alisema.

Akiuliza swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kwa hali ambayo Watanzania wameipata ya mvua ya El-Nino, ni dhahiri utaratibu huo ni mzuri na una tija kwa serikali.

Alihoji kama serikali iko tayari kuhakikisha mfumo huo wa kupeleka dawa vijijini unaharakishwa.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema serikali iko tayari kwa wakati huu kwa sababu njia hiyo ni mkombozi, hasa kutoka ndani ya wilaya kwenda kwenye vituo.

Kumekuwa na changamoto ya dawa kutofika kwa wakati vituoni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiripoti katika taarifa yake ya 2020/21 kwamba baadhi ya vituo dawa zake haziwasilishwi vituoni licha ya kulipa mamilioni kwa Bohari ya Dawa (MSD) au kupokea dawa ambazo muda wa matumizi unakaribia kuisha.




Meneja wa NMB, Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper, akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kulia), vifaa saidizi kwa walimu na wanafunzi wenye ulemavu wa Shule za Msingi Mzambarauni, Uhuru Mchanganyiko, Sekondari za Pugu, Benjamin Mkapa na Jangwani, zote za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, katika ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Walimu (TRC), Wilaya ya Ilala jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa CWT, Andrew Kihako na Ofisa Elimu, Musa Ally (kulia), wakishuhudia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu na wanafunzi wenye ulemavu wapewa vifaa saidizi

**Na Mwandishi Wetu**

WALIMU na wanafunzi wenye ulemavu katika Shule za Msingi Mzambarauni na Uhuru Mchanganyiko na Sekondari za Pugu, Benjamin Mkapa na Jangwani, jijini Dar es Salaam, zimepatiwa msaada wa vifaa saidizi na Benki ya NMB.

Makabidhiano ya vifaa hivyo yalifanyika Alhamisi iliyopita kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Walimu (TRC), wilayani Ilala, jirani na Shule ya Msingi Uhuru Wasichana, ambako Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper alikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo.

Vifaa saidizi vilivyokabidhiwa na NMB kwa Mpogolo, Naye alivikabidhi kwa walimu na wanafunzi wenye ulemavu. Vifaa hivyo pamoja na fimbo nyeupe 60 kwa ajili ya wasioona, lensi 60 za kusomea kwa ajili ya wenye uoni hafifu, kofia 60 na mafuta ya kupakaa chupa 60 kwa ajili ya wenye albino.

Akipokea msaada huo, Mpogolo aliishukuru NMB kwa mchango mkubwa inaotoa kwa serikali kwenye sekta za elimu, afya na majanga.

Alisema benki hiyo imethibitisha kwa vitendo ilivyo na moyo wa kujali jamii, bila kuyasahau makundi maalum ya wenye uhitaji.

Alibainisha kuwa kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), NMB imejipambanua kwa kuunga mkono jitihada za serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufanikisha utoaji elimu bora mijini na vijijini na kuzitaka taasisi, mashirika, kampuni na wafanyabiashara kuiga mfano huo katika urejeshaji kwa jamii.

"Pongezi kwa NMB kwa hakika mko 'serious' sana katika kutumia asilimia moja ya faida yenu kurejesha kwa jamii, ambako mmefanya mambo makubwa kote nchini kusaidia sekta za elimu na afya, huku mkikimbilia jamii ya wenye uhitaji wakati wa majanga.

"Leo (Alhamisi) mko hapa kukabidhi vifaa saidizi kwa walimu na wanafunzi wenye uhitaji maalum kwenye shule zetu kadhaa, hiki mnachofanya ni miongoni mwa matendo ya huruma.

"Kwa niaba ya wanufaika wa msaada huu, nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa matumisi sahihi ya Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii.

"Ndio maana ninaona mnastahili si tu shukrani, bali pongezi kwa kazi kubwa mnayofanya kwa nchi yetu, kwa serikali yetu, kwa wilaya yetu na kwa jamii yetu kwa ujumla.

"Ukitazama benki inayoongoza kwa gawio kubwa kwa serikali ni NMB, benki inayotenga fungu kubwa la CSR ni NMB, hakika mnajali jamii," alipongeza Mpogolo.

Mkuu wa Wilaya akayataka mashirika, kampuni, taasisi na wafanyabiashara kuiga mfano wa NMB katika kutenga na kutumia ipasavyo fungu la CSR, huku akitaka Mamlaka ya Mapato (TRA) kuzibana taasisi zinazorejesha kwa jamii kwa maneno, huku fedha zao zikitumika nje ya urejeshaji kwa jamii.

Naye Prosper aliishukuru serikali na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa kuishirikisha NMB katika kufanikisha upatikanaji vifaa saidizi vya watu wenye ulemavu na kwamba changamoto zinazokwaza ustawi wa elimu na afya ni miongoni mwa vipaumbele vya benki yake kwa kuwa elimu na afya ni mtaji wa maendeleo ya taifa.

"Tunatambua juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kusimamia upatikanaji wa elimu bora kwa nguvu zote kwa kuboresha mazingira ya utoaji huduma hizi mijini na vijijini, nasi tukiwa wadau muhimu, tunao wajibu si tu wa kuipongeza, bali kuiunga mkono kama hivi.

"Hivyo, tuko hapa leo kukabidhi 'Magnfier Lens' 60 kusaidia wenye uoni hafifu, kofia 60 na chupa 60 za mafuta maalum ya kupakaa wenye ualbino, fimbo nyeupe 60 kwa ajili ya wasioona, vifaa ambavyo tunaamini vinakwenda kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu na wanafunzi wetu.

"Tunaishukuru CWT kwa kufikisha maombi yao kwetu, wakiamini na kutambua kwamba NMB ndio mahali sahihi pa kuelekeza changamoto zao na hii inathibitisha namna mnavyothamini mchango wetu kwa jamii, ambako kwa miaka zaidi ya saba sasa tumekuwa tunasaidia kupitia asilimia moja ya faida yetu baada ya kodi," alisema Prosper.

Awali Katibu Mkuu wa CWT Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mahelela, alisema msaada uliotolewa na NMB ni matunda ya chama chake kupitia Kitengo cha Walimu Wenye Ulemavu ambacho kilituma maombi hayo ya vifaa saidizi ili kurahisisha utendaji kazi wa walimu wake.

## Mbunge Musukuma ashtuka miradi ya CSR kutokamilika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Geita (CCM), Joseph Musukuma amesema miradi inayotekelezwa kupitia Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR) katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita haijakamilika licha ya kupokea Sh. bilioni 18 kila mwaka.

Akiuliza maswali bungeni jijini hapa jana, mbunge huyo alisema kuwa kila mwaka halmashauri inapokea Sh. bilioni 4.3 za CSR na kwa mwaka wa fedha 2022/23 zilitengwa, lakini hazikutumika na hakuna wizara iliyokwenda kukagua miradi hiyo.

"Je, Naibu Waziri uko tayari kufuatana na mimi kwenda kunithibitishia miradi uliyoambiwa imekamilika? Kuna jengo linalojengwa na CSR halikamiliki, ni mwaka wa tatu leo," mbunge huyo alihoji.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema halmashauri hiyo imekuwa inapata miradi ya CSR toka kwa kampuni za madini yenye thamani ya Sh. bilioni 4.3 kila mwaka kuanzia mwaka 2018.

Alisema Sh. bilioni 25.8 zimepokewa hadi kufikia Desemba 2023 na miradi 819 imetekelezwa. Kati yake, 661 ni ya elimu, 124 ya afya, tisa ya kilimo na 25 ya sekta mbalimbali.

Naibu Waziri Dugange alisema miradi 653 imekamilika sawa na asilimia 80.

"Kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa CSR kutokukamilika kwa wakati kunakosababishwa na kupanda gharama za vifaa sokoni, ununuzi wa vifaa kufanywa na kampuni na baadhi ya maeneo kutopitika hususani nyakati za mvua.

"Serikali imetunga kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023. Kufuatia kanuni hizi, kamati ya wataalamu imeundwa ambayo itakuwa inapitia miradi na kushauri namna bora ya utekelezaji," alisema.

Alisisitiza serikali inaendelea kupitia kanuni ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kwa thamani ya fedha.





## Ole Sendeka ammwagia sifa Rais Samia

**Na Allan Isack,**
SIMANJIRO

MBUNGE wa Simanjiro, mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ndiye kiongozi pekee wa juu aliyeleta mafanikio makubwa kwa kipindi kifupi alichokaa madarakani.

Alisema kwa uzefu wake wa kushika nyadhifa mbalimbali serikalini nchini hapa nchini tangu enzi ya Baba wa Taifa, Julius Nyerere, hajawahi kushuhudia miradi mingi ya maendeleo inayotekelezwa kama kipindi hiki cha uongozi wa Rais Samia.

Aliyasema hayo juzi kwenye wiki ya Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania, ambapo Benki ya CRDB ilipanda miti 500 kwenye zahanati ya Nakweni iliyoko wilayani Simanjiro mkoani humo, kwa lengo la kutunza mazingira na kurejesha uoto wa asili.

Alisema Rais Samia, amefanikisha utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo kwenye sekta ya elimu, afya maji, umeme na miundombinu ya barabara kwa muda mfupi aliyoongoza nchi kuliko Rais yeyote hivyo mwaka 2025 anapaswa kuongezewa kipindi kingine cha miaka mitano.

Aidha, alisema wana CCM na viongozi wa vyama vya upinzani wanapaswa kujiandaa kisaikolojia wakitambua kuwa Rais Samia ataendelea kuwa Rais wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Nitazunguka maeneo yote ya wilaya na mikoa ya jamii ya wafugaji na kuimba mema yote na mazuri yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan," aliongeza Ole Sendeka.

Hata hivyo, katika tukio hilo, mbunge huyo alituzwa fedha na kalamu ya wino na maaskofu na mashekhe baada ya kughani wimbo wa kumpongeza Rais.

**Alisema kwa uzefu wake wa kushika nyadhifa mbalimbali serikalini nchini hapa nchini tangu enzi ya Baba wa Taifa, Julius Nyerere, hajawahi kushuhudia miradi mingi ya maendeleo inayotekelezwa kama kipindi hiki cha uongozi wa Rais Samia.**

# Wanafunzi wapewa somo kujiepusha na 'mafataki'

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iraqhe, amewataka watoto wa kike hasa waliopo shule za msingi na sekondari kuepukana na vishawishi vya mafataki wanaotaka kukatisha ndoto za safari zao za masomo.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati akizindua Kituo cha Hedhi Salama katika Shule ya Sekondari Themi kilichofadhiliwa na Shirika la Kimaendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wa Wash SDG, kwa kushirikiana na Idara ya Afya ya Halmashauri ya Jiji hilo.

Maximillian alisema mtoto wa kike anapoanza hedhi anakuwa na kutoka kwenye utoto na kuingia utu uzima, hivyo anakumbana na vishawishi ni vingi ambavyo kama wasipokuwa makini wanaweza kuharibia maisha yao.

"Nawapongeza SNV kwa kazi nzuri mliofanya kufungua kituo hiki cha mfano hapa jijini kwetu, lakini mtoto wa kike unapokutana na hedhi umepevuka, kuna vishawishi vya madereva wa daladala, pikipiki, wanafunzi wenzako. Epukeni kupotoshwa na mafataki, kwa hali yoyote angalieni mbele zaidi ili mwendelee na masomo ya juu," alisema.

Aidha aliwataka walimu kubadilisha mfumo wa ufundishaji na kuwafundisha ubunifu wa kazi mbalimbali za mikono, ili wanapohitimu masomo yao, wajiajiri badala ya kutegemea kuajiriwa.

"Soko la ajira kwa sasa wasomi wengi na lipo lile lile haliongezeki, hivyo fundisheni ubunifu watoto ili wafanye kazi mbalimbali kama kupaka rangi, kupiga plasta, kulima bustani, kufinyanga vyungu na mengine mengi, pale mnapokuwa na ujenzi shuleni tumieni hiyo kama fursa ya kufundisha wanafunzi wenu, muandae watoto kujitegemea," alisema.

Naye Kiongozi wa Wash SDG kutoka Shirika la SNV, Olivier Germain, alisema kituo hicho cha hedhi salama kimejengwa kwa zaidi ya Sh. milioni tatu.

Alisema kazi kubwa ya kituo hicho, kutoa elimu ya hedhi salama, kutengeneza taulo za kike ili wanafunzi wanapohitaji wakati wowote wanazipata na kina sehemu ya kujisitiri na kuteketeza pedi zilizotumika.

"Lakini natamani katika nchi za Afrika suala la hedhi lisiwe la kificho, imekua kitu ambacho jamii hukificha kukisema hadharani, natamani kila mtu asimame na kutoa elimu na kua wazi, ili mtoto anapokua shuleni awe huru na asiathirike kisaikolojia, kwa kuona jambo la kawaida," alisema.

Alisema anaamini kituo hicho kitasaidia kuwajenga watoto wa kike kujiamini anapokua shuleni na kufanya vizuri kitaaluma.

Mratibu wa Usafi wa Mazingira na Hedhi Salama Jiji la Arusha, Allan Rushokana, alisema wamezindua kituo hicho cha hedhi salama, ili wanafunzi wote wa Arusha wajifunze masuala ya elimu ya hedhi salama na kueneza kwa wenzao.

"Hapa kwenye kituo hiki mtoto anapata elimu ya mzunguko wake, jinsi ya kujisitiri na jinsi ya kutunza mazingira kwa kuziteketeza kwenye mashine maalum iliyopo hapa ili kutunza mazingira safi," alisema.

Alisema wamechagua Shule ya Sekondari Themi kujenga kituo hicho, kwa sababu ni shule yenye watoto wenye uhitaji maalum ili nao wanufaike na elimu hiyo.

Diwani wa Kata ya Ngarenaro na Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii Jiji la Arusha, Isaya Doita, alipongeza kwa uzinduzi wa kituo hicho ambacho kitatumika kutoa elimu ya hedhi salama kwa shule zote za jiji hilo.



Mkaguzi wa Polisi wa Usalama Barabarani wilayani Muheza, mkoani Tanga, Hebert Kazonde, akitoa elimu ya usalama barabarani katika viwanja vya stendi ya Bombani hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Watakaoshiriki uchaguzi serikali za mitaa wahimizwa kujitathmini

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MONDULI

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM)Taifa, Hassan Wakasuvi, amewataka viongozi wa vijiji, mitaa na vitongoji kujitathmini kabla ya kuchukua fomu iwapo wamewatendea haki wananchi waliowachagua.

Aidha amewataka watumishi wa umma mkoani humo, kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni Ilani ya CCM ya mwaka 2020-25 na siyo kutumia fedha za miradi kwa maslahi yao binafsi.

Wakasuvi alisema hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa CCM kimkoa yaliyofanyika katika viwanja vya Makuyuni wilayani Monduli yenye kauli mbinu ya 'Miaka ya kuzaliwa kwa CCM shiriki uchaguzi kwa uadilifu'.

"Wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji, jipimeni kama mmewatendea haki wananchi waliowachagua kwa kutatua changamoto zao. Ukijiona hukutumiza wajibu wako usijisumbue kuchukua fomu kwa kuwa hatutaki mtu wa kusumbua wanachama wetu," alisema.

Wakasuvi ambaye ni mlezi wa chama hicho, Mkoa wa Arusha, aliwataka wanachama wa chama hicho, kutowaonea haya viongozi ambao hawakufanya kazi kwa kipindi cha miaka mitano kuwaambia ukweli kuwa wasichukue fomu.

Aliwasihi wakiona viongozi wenye sifa ya kugombea nafasi hizo katika mtaa, vijiji au vitongoji vyao wawashawishi kuchukua fomu na kumfanyia kampeni ili ashinde kwa maendeleo yao.

Katika hatua nyingine, Wakasuvi alisema kamati za uteuzi wa wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa wanatakiwa kutenda haki kwa wagombea wote ili kuepuka malalamiko yasiyo na sababu.

Awali Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Loy Thomas Ole Sabaya, alisema chama hicho katika mkoa huo, kimejipanga kikamilifu kutatua changamoto zote zinazowakabili wananchi kwa kushirikiana na serikali ikiwa ni pamoja na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 katika mkoa huo.


Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa ya kuleta fedha za miradi ya maendeleo mkoani humo, ambapo katika sekta ya elimu wa kipindi cha miaka mitatu wamepokea Sh.bilioni 47 kwa ajili ya kukarabatiwa na ujenzi wa shule mpya za msingi 16 na sekondari mpya 25.

Mongella, alisema katika sekta afya kwa kipindi hicho, wapataa Sh.bilioni 32.8 pamoja na vifaa tiba vyote muhimu ambapo kwa sasa dawa zote muhimu zinapatikana kwa zaidi ya asilimia 92 kwa mkoa mzima.

"Rais Samia amefanya kazi kubwa katika kutatua changamoto za wananchi wa Mkoa wa Arusha ambapo tumejenga zahanati 45, vituo vya afya 18 katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hospitali saba za wilaya ambazo zinatoa huduma za kibingwa," alisema.

Kuhusu sekta ya barabara Mongella, alisema Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), wamepokea Sh.bilioni 39 ambapo katika halmashauri zote za Mkoa wa Arusha ujenzi wa miundombinu ya barabara unaendelea.

Alisema pia wamepokea Sh.bilioni 78 kuboresha miundombinu ya umeme ambapo vijiji 329 vimeshapata umeme vimebaki vijiji saba pekee na mkandarasi anaendelea na kazi.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Serikali yaagiza waliogomea fidia ya nyumba walipwe fedha

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imeuagiza Mgodi wa Almasi Mwadui, kuandaa utaratibu mzuri wa kuwalipa wananchi wanne kati ya 47 waliogoma kujengewa nyumba kama fidia, wakitaka walipwe fedha.

Mgodi huo ulilazimika kuwalipa wananchi hao kutoka Kijiji cha Mwang'holo wilayani Kishapu baada ya nyumba zao kuvamiwa na maji tope yaliyotoka kwenye kampuni yao.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alitoa agizo hilo juzi wakati akizindua na kukabidhi nyumba 42 kwa wananchi waliosalia kulipwa fidia ya ujenzi wa nyumba na mgodi huo.

"Wananchi hawa wanne ambao wamegoma kabisa kujengewa nyumba za fidia, andaeni utaratibu mzuri ukiwamo wa kimaandishi na muwalipe pesa zao," alisema Mndeme.

Aliwataka wananchi kutunza mazingira kwa kupanda miti na kuagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wilayani Kishapu na TANESCO, kupeleka huduma za maji na umeme eneo hilo.

Meneja Mahusiano mgodi huo, Bernard Mihayo, akitoa taarifa ya ujenzi wa nyumba hizo, alisema waathirika 47 ndiyo walipoteza nyumba zao, na tayari nyumba 42 zimekamilika na wameshakikabidhi kwa wahusika.

Mihayo alisema tararibu na mazungumzo yanaendelea kwa wale waliokataa kujengewa nyumba na watalipwa kulingana na hali ya nyumba zao za tembe zenye thamani ya Sh.milioni 1.8.

Alisema hatua inayofuata ni kuhamisha makaburi 14 ya waathirika wa majitope, pamoja na kuwaanzishia miradi ya kuwaboresha vipato vyao ikiwamo ufugaji wa kuku na mbuzi.

Baadhi ya wananchi waliogoma kujengewa nyumba za fidia akiwamo Maimuna Kasara, alisema anahitaji kulipwa fedha kwa sababu hataki tena kuendelea kuishi katika eneo hilo.

Novemba 7, 2022 bwawa la majitope katika Mgodi wa Almasi Mwadui wilayani Kishapu lilibomoka na tope kwenda kwenye makazi ya watu likisababisha madhara mbalimbali.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akicheza pamoja na Jeshi la Jadi Sungusungu wakati likitumbuiza juzi kwenye Sherehe za Polisi 'Family Day' mkoani Shinyanga, alilitaka jeshi hilo kuongeza kasi ya kudhibiti ajali za barabarani ambazo zimekithiri mkoani humo, na uhalifu ili mkoa uendelee kuwa salama. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Visima virefu vyatokomeza kipindupindu Bariadi

**Na Ndalike Sonda,**
BARIADI

WANANCHI katika Kijiji cha Nyanguge, Kata ya Ngulyati wilayani Bariadi mkoani Simiyu wametaja uwapo wa visima virefu vya majisafi vinavyotumia umeme katika kijiji hicho kuchangia kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu ulioibuka hivi karibuni.

Visima hivyo vya kuchimba vyenye maji yaliyotibiwa kwa dawa aina ya Klorini vimejengewa mabomba kwa ajili ya kusambaza maji katika baadhi ya vijiji ikisaidiwa na umeme wa REA.

Wakizungumza na Nipashe juzi baadhi ya wananchi hao walisema kuwa upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yao umewapa uhakika wa kuwa na afya salama kwa kuwasaidia kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu tofauti na ilivyokuwa hapo awali walipokuwa wanatumia maji yasiyo salama.

Mkazi wa Kijiji cha Nyanguge, Leah Mabula, alisema awali walikuwa wanahangaika kufuata maji umbali mrefu ambayo hata hivyo hayakuwa salama kwani walikuwa wakitumia maji ya kwenye milima na madimwi.

Naye John Nshashi alisema walikuwa wakitumia muda mrefu kufuata huduma hiyo kulikosababisha uchumi wao kushuka na tishio la magonjwa ya mlipuko. Mwenyekiti wa kamati ya maji kutoka kata ya Ngulyati, Swales Ngusa, alisema kuwa awali mradi huo ulikuwa ukitumia gharama kubwa katika uendeshaji wake lakini tangu walipounganishiwa na huduma ya umeme kutoka mradi wa REA, umesaidia kupungua gharama za uendeshaji.

Ofisa Afya na Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma Mkoani, Simiyu Salum, alisema maji hayo ni safi na salama kwa afya ya binadamu kwani yametibiwa ili kudhibiti vimelea visababishavyo magonjwa ya mlipuko ikiwepo kuhara na kutapita.

Kijiji cha Nyanguge ni miongoni mwa vijiji kumi vilivyonufaika na mradi huo kutoka Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati ya Umeme Vijijini (REA) kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Lengo la mradi huo ni kupambana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na UVIKO-19 na kusambaza umeme katika visima ambavyo havikuwa na pampu za umeme za kuvuta maji.

# Wahitaji ushirikishwaji kudhibiti kipindupindu

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, amesema kuna haja ya wananchi, madiwani na wadau wa afya kuungana kwa pamoja ili kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu unaoendelea kuzikabili jamii katika halmashauri hiyo.

Alisema wamekuwa wakipokea wagonjwa 15-20 kwa siku na hadi kufikia Februari 2, 2024 wagonjwa wapya walikuwa ni 22 kati yao 21 wanatokea wilayani hapa.

Dk. Rutachunzibwa aliwaomba madiwani kuunga mkono jitihada za serikali kwa kuenda kutoa ushirikiano kwa viongozi wa vijiji na vitongoji kwa kufanya usafi na kutumia maji tiririka ili kuondokana na kipindupindu.

Akizungumza katika Baraza la Madiwani la kujadili rasimu ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisa Operesheni za Dharura za Afya ya Jamii kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Erenest Kyungu, alisema wanatakiwa kushirikisha na kutoa elimu kwa wananchi ikiwamo usafi.

Aliwahimiza madiwani kuendelea kutoa elimu katika mazingira ambayo wanaishi badala ya kuiachia Idara ya Afya pekee lakini pia kuhakikisha wanafuatilia kile ambacho kinaendelea katika eneo lao.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliomba kila mmoja kusimamia suala hilo kwa nafasi yake kuhakikisha usafi unafanyika kwa hali ya juu ikiwamo kukomesha utiririshaji ovyo wa majitaka kwenye makazi ya watu hali inayoifanya wilaya hiyo kuzidi kuwa na maambukizi mapya.

Diwani wa Kata ya Chifufu, Robath Madaha ambaye eneo lake limeathirika kwa kiasi kikubwa na ugonjwa huo aliahidi anatoa elimu kwa wananchi namna ya kujikinga na kuhakikisha tatizo hilo la kipindupindu linaisha.

Mlipuko wa kipindupindu katika Wilaya ya Sengerema ulianza Januari 30, 2024 ambapo hadi kufikia Februari 2, 2024 waliripotiwa kufikia wagonjwa 21 wanaoendelea kupatiwa matibabu katika vituo vya afya.

Sophia John ni mkazi wa Ibisabageni alisema kipindupindu kilikuwapo tangu kipindi cha mababu na tayari wamepata elimu na watahakikisha wanakuwa wasafi na kutunza mazingira.

Katika Baraza hilo madiwani walipitisha makadirio ya bajeti ya Sh. bilioni 3.3 kwa ajili ya mapato ya ndani pamoja na OC kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 6 , 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12

Wazazi, walezi mnapokimbizana na shule msiwasahau wenye usonji


Ukurasa 13

Unapopambana na 'red eyes' usisahau kujihadhari na ugonjwa wa vikope


Ukurasa 14

**Hawa wana miaka na kalenda zao, mwaka 2024 si kwa kila mtu**

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

MISIBA EL-NINO

# Matokeo ya undumilakuwili kwa wanasiasa na watendaji

## •Athari zinazotokea leo ni kupuuza wataalamu, sheria



Mabadiliko ya tabianchi yalivyosambaza mafuriko sehemu mbalimbali Afrika. **PICHA: WFP**

WENGI wameshuhudia namna ambavyo mvua ya el-nino, ilivyoleta maafa kuanzia vifo na uharibifu mkubwa wa miundombinu mijini na vijijini, ukweli ni kwamba chanzo ni kuharibu mazingira na kupuuza sheria.

Mazingira ndiyo yenye misitu, maji, hewa, viumbe hai, mimea ya aina zote na yote hayo yanasimama juu ya ardhi ambayo ni nguzo muhimu kwa uchumi na maendeleo ya taifa.

Bila kuwapo ardhi hakuna maendeleo ya viwanda wala makazi hivyo, inabidi kuwa makini na matumizi bora na endelevu ya ardhi katika taifa na kuilinda sheria.

Kwa upande mwingine, mazingira huharibiwa kutokana na matumizi yasiyorafiki hususani maeneo karibu na kingo za mito, mikondo ya maji, maziwa na mabwawa pamoja na kwenye mbuga za wanyama au maeneo ya wazi yanayohifadhiwa kisheria.

Uharibifu wa ardhi haufanywi na mtu mmoja mmoja au wananchi wasio na uelewa hata baadhi ya viongozi wanachangia kwa kiasi kikubwa, kuharibika mazingira sehemu mbalimbali na kuwa chanzo cha maafa kama mvua za mwaka huu.

Uzoefu wa miaka mingi unaonyesha kuwa hoja au ushauri kutoka kwa wataalamu havizingatiwi na baadhi ya wenye kufanya maamuzi au kutunga sera, sheria na mipango ya kisiasa na au wanaosimamia utekelezaji wake.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hupelekewa miswaada ambayo huijadili na kupitishwa rasmi. Baada ya hapo hupelekwa kwa Rais na kuwekwa saini na kuwa sheria ambazo hutayarishiwa kanuni na hatimaye kuanza kutumiwa.

Ajabu ni kwamba watu wachache, wenye mamlaka wakiwatetea wanaovunja sheria au kanuni, mfano, kuanzisha makazi sehemu ambazo hawatakiwi kufanya hivyo au kulima au kuchunga mifugo kwenye maeneo yanayosimamiwa kisheria.

Mamlaka za Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wanapojaribu kutekeleza sheria, wenye madaraka au viongozi huwazuia wasiwaondoe wananchi sehemu walizovamia kwa kisingizio kuwa 'wanaganga njaa'au hawana sehemu nyingine za kuanzisha makazi.

Hata wananchi nao wamefahamu udhaifu huo hivyo, inapokaribia nyakati za uchaguzi hujisogeza na kuvamia maeneo yaliyohifadhiwa kisheria.

Lakini wanafanya hivyo wakifahamu kuwa hawatatolewa maana watalindwa na baadhi ya viongozi. Wakati mwingine kiongozi anadiriki kuwaruhusu walime au kuanzisha makazi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kisheria kwa kuahidi kuwatetea.

Wataalamu au watekeleza sheria wakiona wamezidiwa na wakubwa wananyamaza na matokeo yake ni kama inavyoshuhudia sasa mahangaiko makubwa kutokana na mvua zinaponyesha kwa wingi maisha na rasilimali hupotea.

Kwa hali hiyo, mvua kubwa imenyesha, maji mengi yanatiririka kwa kasi kubwa, kiasi cha kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuusafirisha hadi mabondeni mpaka kwenye vijito, mito na mikondo ya maji.

Maeneo ya mijini mfano Dar na Morogoro, maji husafirisha takangumu na majitaka hadi kuziba mitaro hivyo kushindwa kupitisha maji na kuleta hatari barabarani na maeneo kadhaa kutokana na mafuriko yasiyotarajiwa.

Mchakato wa mvua kusafirisha udongo au mchanga na takangumu unapochukua miongo kadhaa husababisha vina vya mito au mabwawa na maziwa kuwa juu kiasi cha kupelekea mafuriko kutokea haraka kama ilivyoanza Novemba, 2023 hadi leo el-nino, ikishuhudiwa kwenye Mto Msimbazi na mito mingine mingi ya Dar-es-Salaam.

Isitoshe athari za mvua kubwa zimejitokeza sehemu mbalimbali nchini kiasi kwamba matukio kama hayo yanatia simanzi mioyoni mwa Watanzania wengi. Ni vyema kujifunza wasikubali yaendelee kujitokeza kwa kuchukua hatua mapema kuyadhibiti ipasavyo, hata yakitokea iwe ni utaratibu wa maumbile lakini si wananchi.

Athari za mazingira kwa Mto Msimbazi ni kitendawili tena cha siku nyingi. Kanuni za sheria ya mazingira, pamoja na sheria ndogo za halmashauri au serikali za mitaa, zinatakiwa kulinda mazingira ya mito na vijito yasiharibiwe kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu wanaoishi karibu na vijito au mito na mabonde yenye kujaa maji mara kwa mara wakati wa mvua za vuli na masika.

Mathalani, kanuni inayoainisha kuwa kutoka kwenye kingo za mito mikubwa mfano Msimbazi, Ruvu, Wami ni hadi mita 60 shughuli zozote za kibinadamu iwe ni kilimo, ufugaji au makazi zisifanyike ndani ya ukanda huo.

Kwa mito midogo eneo hilo hupungua hadi mita 30, lengo la kuhifadhi maeneo hayo ni kuhakikisha kunakuwepo na uotoasilia wa kutosha ili kuzuia kasi ya maji ya mvua yasipeleke udogo au mchanga, matope na takataka nyingine kwenye mito au vijito.

Lakini, pia kulinda maji yabaki salama wakati wote hivyo kupunguza gharama za kuyasafisha kabla hayajasambazwa kwa wateja

INAENDELEA UK.12

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

# Wazazi, walezi mnapokimbizana na shule wakumbukeni wenye usonji

MWEZI unaelekea ukingoni tangu shule ilipofunguliwa kwa wanafunzi wa msingi na sekondari. Mzazi au mlezi watoto wanahitaji kusoma bila kujali wana upungufu au changamoto za kimaumbile, hivyo waangalie wenye mahitaji maalum wakiwamo wenye usonji.

Katika kulihudumia kundi hili la wenye usonji, ambalo wengi huwaita watoto wenye utukutu ni vyema kuwahi hospitalini au kwa wataalamu wa afya ya akili inapoonekana mtoto ana dalili ambazo ni tofauti na zile zinazofahamika ili kupata ushauri mapema.


Ukiwafikisha kwa wataalamu watafahamika iwapo wana usonji na kwa kiwango au ukubwa gani.

Kama unavyojibidiisha kuwapeleka wale wenye utimamu wa maumbile na afya shuleni, wapeleke pia wenye usonji kujifunza wakiwa na umri mdogo ili kupata ujuzi ambao wataalamu wanashauri.

Skili hizo ni pamoja na za kuwasiliana, kuwa na utulivu na kujichanganya na wana jamii.

Ikumbukwe usonji au autism ni ugonjwa wa mishipa ya fahamu au neva kwenye hatua za kukua unaoathiri namna binadamu anavyoshirikiana na wenzake kwenye kuwasiliana, kujifunza, kujichanganya na jamii.

Usonji unagundulika katika hatua za mwanzo za ukuaji wa mtoto lakini na katika umri wowote, japo huonekana katika miaka miwili ya mwanzo, hivyo ni vyema kuchunguza na kumsaidia mtoto.



Baadhi ya wazazi wa watoto wenye usonji wanatuma salama zao kwa wengine, wakiwashauri wenye watoto hao wasiwafungie ndani wala kuwapiga, kuwanyanyasa na kuwatesa.

Wazazi na walezi wanahimizwa kujitahidi wawezavyo kuacha kumfanya mtoto aone kuwa usonji ni jambo baya au ni kuwa na kasoro.

Wakati mwingine wenye usonji wanafikiri kuwa wana tatizo au wako tofauti na wenzao, ni kutokana na mazoea ya kuongea kwa kejeli na unyanyapaa dhidi yao.

Wanasema kuwa kwa kiasi kikubwa huanzia ndani ya wanafamilia wanaowatukana, kuwanyanyapaa kwa kuwa hawana uewelewa kuhusu usonji, lakini leo mzazi au mlezi anayefahamu asiendeleze mambo hayo.

Wanasema hakuna sababu ya kuwatukana, kuwafokea na kutoa maneno mabaya dhidi yao na ikiwezekana kukomesha mienendo hiyo.

Mfano mzazi mwenye watoto wawili wenye usonji, anasema licha ya mkubwa kuwa na miaka nane bado anavaa pempasi na hajaweza kuzungumza wa pili alipozaliwa naye alikuwa na changamoto hiyo ya kutokuzungumza na alipofikishwa kwa daktari alibainika ana tatizo la usonji.

Anakumbusha kuwa jamaa zake walianza kusema kwa sababu kaka mkubwa hazungumzi ni dhahiri hata mdogo naye atakuwa bubu kwa sababu maji hufuata mkondo.

Wazazi na walezi wenye watoto hawa wanakumbushwa wasibadilishe utaratibu wa maisha ya kuwahudumia watoto kwa ghafla.

Mfano, ukiwapa chai au chakula saa 2:30 asubuhi usibadilike ukaanza mapema au ukachelewa maana kile unachowafundisha ndicho wanachokamata.

Watoto wengi wenye hali hiyo wameimarika katika mpangilio wako au uliowazoesha na umekuwa kawaida kwao hivyo uzingatie. Hata kama italazimika kubadilisha utaratibu kwa ghafla, wazazi wao wanapaswa kufanya kwa utaratibu ili kuhakikisha kwamba mtoto mwenye usonji anabaki na hali yake aliyoizoea asibadilishiwe mambo yake pasipo ulazima.

Mabadiliko ya mara kwa mara yanaweza kusababisha hisia kupita kiasi, wapo wanaoweza kuzoea vizuri zaidi wakati mwingi, japo wengi hupambana na mabadiliko na hawako tayari kubadilika, hata wakifanya hivyo ni kwa muda mrefu.

Ikumbukwe kuwa mabadiliko ya ghafla yanakuwa ni jambo kubwa zaidi kwake na yanasababisha mfano ashindwe kulala kwa kukosa usingizi na wakati mwingine inashindikana kumfariji na kumfundisha.

Wazazi na walezi wanaaswa wasiwalinganishe na wengine na kuwasemea lugha ya kuwanyanyapaa.

Wazazi wenye uzoefu na watoto wenye usonji wanawakumbusha wengine kuwa wasiongee kwa mafumbo au lugha isiyoeleweka, au isiyonyooka, mfano mtoto anakuuliza mama niweke wapi sahani hii?

Unamjibu kichwani, ataibandika kichwani. Hivyo ni vizuri kuwa makini na kutoa mafundisho yanayoeleweka na yenye ukweli na manufaa.

Baadhi ya watoto wenye usonji wanataabika kutumia lugha za mafumbo au zenye ugumu ikumbukwe wanaweza tu kuona mambo kwa maana halisi ambayo wanaieelewa baada ya kufunzwa na kuwapa mafumbo au lugha zisizoeleweka ni kuwachanganya.

Usiwafokee au kuwakimbilia fanya mambo kwa hatua na kwa upendo. Kama wazazi au walezi kuwa na watoto wako muda wote. Wawe kwenye akili yako mara kwa mara.

Ongeza juhudi kutambua kama kuna magonjwa ya akili kwa mtoto au watoto wako, kumbuka wanaweza kuatharika zaidi ikiwa utapoteza utulivu nao.

Wanaoishi na watoto hawa hasa wazazi, inaweza kuwa vigumu kuwa mtulivu wakati mtoto anahangaika. Unaweza kuongea naye kwa utulivu na kumfanya ajibu kwa utulivu pia maswali unayomuuliza akayamudu ukiwa wewe ni mtulivu.

Kudumisha utulivu kunaweza kukusaidia wewe na mtoto wako aliye na usonji kuwasiliana vyema na kukuza uhusiano bora.

Usiwaache watoto wenye usonji kwa muda mrefu wenyewe au bila mtu wa kuwasikiliza ikiwamo kuwasaidia. Ingawa watoto wengi wenye usonji wanaweza kuishi kwenye utaratibu wao wenyewe, bado hawapaswi kuachwa bila kufuatiliwa na kutunzwa kwa muda mrefu.

Ni vizuri kuwafuatilia kwa sababu katika kucheza kwenye eneo au chumba chao au kwenye uwanja wao wanaweza kupata hatari zilizofichwa na kuzifuata hata wakaumia.

Ni jukumu la wazazi na walezi kuhakikisha kuwa tunawachunguza na kuwafuatilia kila mara na kuona kama kuna hali ambapo usimamizi haupatikani kwa muda ni vizuri kuweka njia mbadala na salama.

Unapowafundisha kufahamu mambo na shughuli mbalimbali wape majukumu mepesi usiwarundikie kazi ngumu ambazo hawataweza kuzigusa.

# Matokeo ya undumilakuwili kwa wanasiasa na watendaji

**INATOKA UK.11**

mijini, Hata hivyo, kutokana na matamko ya baadhi ya viongozi ambayo ni kinyume na sheria au kanuni kwa sababu wanazozijua wenyewe, wananchi huchangamkia fursa kadri wanavyoona inafaa bila kujali matokeo hasi kwa mazingira ambayo manufaa yake ni kwa watu wengi. Kawaida Mto Msimbazi unapoingiza maji baharini, unapita sehemu ambayo, kutokana na asiliyake ni mahali pa bahari kupumua wakati wa wimbi la juu ambalo hutokea mara mbili kwa siku takribani saa 3 asubuhi na nyakati za alasiri.

Wakati hayo yakitendeka, maji yenye chumvi kutoka baharini na baridi yasiyo na chumvi yakielekea baharini hufika mahali yakachanganyika, kwenye mwalo wa bahari, ambako ya chumvi na baridi hukutana.

Mchanganyiko huo ni tukio asilia kwa miaka yote tangu kuumbwa dunia na maeneo kama hayo kiasili huwa yamezingirwa na ardhioevu yenye uoto wa asili wa miti ya mikoko inayostawi kwenye majichumvi.

Sehemu nyingine zinazoambatana kama ilivyo kwa mazingira ya Mto Msimbazi ni Rufiji Delta kwenye Mto Rufiji huko mimea mingine yenye asili ya ardhioevu isiyo na majichumvi huweka mazingira ya mito katika uhalisia wake.

Hali ya mazingira kwenye Mto Msimbazi, ndivyo ilivyo kwa mito yote inayomwaga maji baharini. Kadhalika, maeneo ya mito inayoingiza maji baharini yamesheheni ardhioevu ambazo hazitakiwi kufanyike shughuli za aina yoyote.

Wakati wa ujenzi wa barabara zinazokatiza katika maeneo kadhaa ya Mto Msimbazi ikiwamo ya Morogoro tahadhari ilitolewa kwamba mara ujenzi ukikamilika kusifanyike shughuli nyingine za kibinadamu isipokuwa zisizo na athari kwa mazingira kama mikutano ya hadhara au utalii asilia kwa ajili ya kufurahia mandhari.

Juhudi za wataalamu, wasimamizi wa sheria au kanuni za mazingira ili kuzuia uharibifu usiendelee, zimekuwa zikikwamishwa na wenye mamlaka.

Kadhalika, wakati wa ujenzi miundombinu ya mabasi-mwendokasi, wataalamu walitahadharisha kuwa kwenye ardhioevu ya Mto Msimbazi kusijengwe kituo cha mabasi ya mwendokasi kwa kuwa ni eneo muhimu kwa bahari kupumua.

Aidha wakati maji yakiwa mengi eneo hilo hutumika kuyadhibiti yasilete madhara makubwa. Yote yaliingia kwenye sikio la kwanza yakatokea la pili.

Taifa linaingia gharama kubwa ya kuondoa udongo na mchanga na takangumu kwenye mito na wakati mwingine, wasafiri kuhangaika kutokana na babarabara kuharibika mfano, mabasi ya mwendokasi kushindwa kupita sababu ya barabara kujaa maji.

Yote hayo ni uthibitisho kuwa wataalamu hawasikilizwi na baadhi ya wakubwa wanaofanya maamuzi yanayopingana na ushauri unaotolewa na wasimamizi wa masuala ya ulinzi wa rasilimali na mazingira.

Halikadhalika, kilimo kisichokuwa endelevu hasa kufyeka misitu, kuichoma moto na kuchunga mifugo bila kuzingatia kanuni za matumizi bora ya ardhi, kumekuwapo na changamoto za uharibifu wa ardhi hivyo kusababisha maeneo mengi kuwa wazi bila uoto wa asili. Hali hiyo, huchochea mmomonyoko wa udongo kupitia kasi ya maji ya mvua pamoja na nguvu ya upepo mkali, kupeperusha chembechembe za udongo na kuzipeleka mabondeni hadi kwenye mito, mabwawa na katika maziwa.

Kwa hiyo kila mmoja ajifunze mvua inayonyesha iwe sehemu ya darasa na kujirekebisha na kutunza mazingira.

ELIMU

NA WAANDISHI WETU

# Unapopambana na 'red eyes' usisahau kujihadhari na ugonjwa wa vikope



Kinamama wakichunguzwa vikope. **PICHA: MTANDAO**

MARADHI ya macho au 'red eyes' yamesambaa sehemu mbalimbali, yakiwaumiza watoto kwa watu wazima. La muhimu ni kuwahi hospitalini na si kujitibia kienyeji mitaani.

Wakati red eyes ikibapamba moto yapo maradhi ya vikope au trakoma ugonjwa uliosahaulika lakini wenye madhara kwa jamii.

Vikope husababishwa na vimelea viitwavyo 'klamidia' lakini husambazwa na nzi na visipotibiwa mapema husababisha kope kupinda na kuingia ndani, kukwaruza kioo cha jicho na hatimaye upofu.

Trakoma huenezwa na nzi anayebeba vimelea kutoka kwenye jicho lenye maambukizi kwenda kwa asiye na maradhi.

Huambukizwa kwa njia tofauti kama kugusa macho ya vikope kisha kugusa macho ya mtoto asiye na maambukizi, au kugusa macho yako mwenyewe au kushika uso bila kunawa.

Lakini, pia kupeana au kushikana mkono na aliyegusa vimelea au mwenye trakoma halafu ukashika uso au macho bila kunawa na sabuni.

Kadhalika husambaa kwa kushirikiana taulo, kanga na vitambaa vya kukaushia mwili au mikono ikiwa kuna mmoja mwenye ugonjwa huo.

Maambukizi yapo zaidi maeneo yasiyo au yenye upungufu wa maji safi na salama, mazingira machafu, kutokutumia choo na kujisaidia ovyo na kutupa kinyesi cha watoto kwenye mazizi ya mifugo, vichakani au karibu na nyumbani.

### DALILI

Ni pamoja na macho kuuma, kuwasha, kuhisi kama yana mchanga, kutoka machozi, kuwa mekundu, kujaa matongotongo, kutostahimili mwanga, na kope kugeukia ndani na kukwaruza kioo cha jicho, makovu kwenye kioo cha mbele cha jicho, kutoona vizuri na kupofuka.

Ugonjwa huu duniani ni kati ya maradhi mengi yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, hata hivyo, kuanzia miaka ya 2000 kumekuwa na msukumo na juhudi za kupambana zaidi.

Juhudi hizo ni pamoja na kampeni za kutoa dawa kwa magonjwa ambayo hayapewi kipaumbele na kwa kipekee kutoa tiba kinga ya dawa ya Zithromaxh, kukinga jamii dhidi ya trakoma.

### MADHARA YAKE

Ugonjwa huu huendelea kuwa ndani ya mtu kwa muda mrefu na kusababisha kupata upofu asiweze kuona tena. Takwimu za vikope zinaonyesha kuwa karibu watu milioni 1.9 wana uoni hafifu kwasababu ya trakoma na pia asilimia 1.4 ya hao wamekuwa vipofu.

Tanzania imeshuhudia madhara ya ugonjwa wa vikope ikiwa pamoja na kuongezeka kwa matatizo ya macho, uwezo mdogo wa kujifunza kwa watoto shuleni, kupofuka na vifo ambavyo mara nyingi si rahisi kugundua.

Trakoma huleta madhara kimya kimya kwenye afya za wanajamii ikimaanisha huua kimya kimya bila hata mwenye kuathirika kuelewa.

Mfano, tatizo la ugumba ni vigumu kutambua kuwa ni sababu ya ugonjwa wa vikope ambao haukutibiwa kwa wakati hivyo leo kuleta madhara makubwa kwenye uzazi.

Madhara ya trakoma yameleta matatizo makubwa kwenye nguvukazi ya taifa hasa pale mwanajamii anapokuwa kipofu na kushindwa kuendelea na majukumu ya uzalishaji mali, aidha trakoma imeathiri na kurudisha nyuma maendeleo kiuchumi na kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

### CHA KUFANYA

Ugonjwa huu unaepukika kwa kubadili tabia mbaya na kuendeleza zenye kujikinga.

Kwa mfano, kuishi kwenye mazingira yasiyo safi, kutokunawa mikono na uso kwa sabuni, kushirikiana nguo za kujikaushia kama taulo na vitambaa.

Baadhi ya hatua za kuchukua ni pamoja kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huo, umuhimu wa kuwahi kituo cha tiba kupata matibabu.

Kuwahi mapema kabla tatizo halijawa kubwa zaidi au kufikia hatua ya kushindwa kutibika hasa pale upofu unapotokea.

Aidha, kujitahidi kufuata ushauri unaotolewa na watoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na kuzuia hasa watoto kushika na kushirikiana vitambaa kama leso na taulo.

Kuhimiza kunawa mikono, kunywa maji na kula chakula safi na salama, kupumzika vya kutosha, kuzingatia lishe na mlo kamili ili kuupa mwili uwezo wa kupambana na maradhi mbalimbali pamoja na kufanya mazoezi.

Kuzingatia masharti na maelekezo ya wataalamu, hasa wale waliopimwa na kugundulika na vikope na kutibiwa, ikiwa ni pamoja na kutumia dawa kwa wakati na kwa usahihi. Pia kuzingatia ushauri wanaopewa na wataalamu wa afya.

Kadhalika serikali iendelee na juhudi za kuongeza huduma za majisafi na salama ili jamii isikose maji.

### FAIDA

Watanzania wanakumbushwa kuwa kama kila mmoja atachukua hatua sahihi za kujikinga lakini iwapo akiambukizwa kupata matibabu ya ugonjwa wa trakoma, taifa linategemea kupata faida nyingi.

Mfano kuanzia kwa mtu binafsi, jamii na taifa na ya kwanza ni kuwa kila mwanajamii na jamii nzima itakuwa yenye afya njema hivyo kuwa na muda wa kutosha katika kufanya na kushiriki shughuli za maendeleo.

Pili ni taifa na jamii kuepuka gharama na muda ambavyo vingetumika katika kutibu ugonjwa wa vikope au trakoma.

Gharama hizo ni fedha na muda bila kusahau uhai wa watoto na watu wazima wanaokufa kwa ugonjwa huo.

Pamoja na faida hizo nyingine ni kuandaa kizazi kijacho chenye afya njema kwani waathirika wakubwa wa ugonjwa wa vikope ni watoto.

Hivyo kulinda kundi hili dhidi ya ugonjwa huu ni kuandaa kizazi bora kijacho chenye uwezo wa kushiriki katika harakati za maendeleo.

Mambo hayo yataiwezesha jamii na taifa kuwa na raia wenye afya njema na kufikia maendeleo wanayoyatarajia na kuyatamani kwa wakati kadiri ya mipango ya nchi.

Ni wazi kuwa kila mmoja amefahamu umuhimu wa kuchukua hatua za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa vikope au trakoma katika ngazi ya mtu binafsi na katika ngazi ya jamii.

Hivyo huu ni wakati wa kila mmoja kutimiza jukumu hilo kikamilifu na kuchukua hatua za kujilinda na tahadhari huku akiishi maisha ya afya na kujiepusha na maradhi.

Wito wetu kwa Watanzania ni kumtaka kila mwananchi aanze kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa vikope ili kujinga na kuchukua hatua mapema kujikinga na jamii inayomzunguka hasa watoto.

Hii ni pamoja na kuhakikisha watoto na watu wazima wananawa majisafi, kusafisha mazingira ikiwa ni pamoja na kuondoa wadudu wale wanaosambaza ugonjwa hasa maeneo ya vyanzo vya maji.

Aidha, serikali iongeze juhudi katika kupatikana majisafi na salama kwa jamii hasa katika maeneo yenye hatari zaidi ya kuwa na ugonjwa wa vikope nchini.

Kadhalika, wataalamu wa afya watoe elimu kwa jamii kuhusu tatizo la ugonjwa wa vikope, madhara yake na namna ya kujikinga pamoja na kutembelea vituo vya huduma za afya mapema ili kupata msaada na tiba ya ugonjwa huo.

Kama kila mmoja popote alipo atafanya hivyo itafanikisha wananchi kupunguza madhara yanayoletwa na ugonjwa huo.

Aidha, pamoja na watoto kukosa kuhudhuria shule kutokana na kuugua vikope, familia na jamii kutumia fedha nyingi na muda katika kutafuta na kupata matibabu badala ya kuwekeza kwenye shughuli za maendeleo.

Kama jamii itafanya haya yote, huenda taifa likapata suluhisho la muda mrefu hasa katika kuhakikisha afya ya kila Mtanzania hasa mtoto inakuwa katika hali njema muda wote.

**Waandishi:Dk. George Kabona na Stephen Mbwambo, Wizara ya Afya.0752-814803.**

**Pankras Luoga: Mhadhiri Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS)-0757645746.**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Hawa wana miaka na kalenda zao, mwaka 2024 si kwa kila mtu

## • China, Iran wamo kwa Waethiopia leo ni 2016

KOKOTE uliko iwe kijijini au mjini, ndani ya daladala au darasani, ikiwa unachati mitandaoni au kusikiliza redio unafahamu kuwa leo ni Jumanne Februari 6, 2024.

Ndiyo kalenda inayokuongoza kujua siku na miezi kwa mwaka huu. Kalenda inayotumika ilipangwa na Papa Gregory wa 13, Kiongozi wa Kanisa Katoliki, ndiyo inayofuatwa na karibu nchi nyingi dunia nzima.

Inaiitwa Gregorian Calendar ikitengenezwa na Papa aliyezaliwa mwaka 1502 na kufariki 1585, akiwa na miaka 87.

Hata hivyo licha ya kuendelea kuitumia na kuifikisha dunia mwaka 2024, tena ikitimiza miaka 442 tangu kuandaliwa, siyo wote wanaoitumia.

Kuna baadhi ya mataifa mengine yenye kalenda zao zenye mwaka, siku na miezi tofauti na Gregorian.

Kalenda ya Gregorian inayokubalika katika nchi nyingi inafuata mzunguko wa jua, imefanyiwa marekebisho ya kalenda ya Julian, kiongozi wa Kirumi, mashuhuri Julius Caesar, ambayo ilikuwa inafuata mzunguko wa dunia kuzunguka jua, ikidaiwa haikuwa sahihi.

Wakati huo nchi za Kikristo zilisherehekea mwaka mpya Machi 25, tarehe inayoelezwa kuwa malaika Gabrieli alitumwa kwenda kwa Bikira Mariam kumweleza kuwa atamzaa Masiha Yesu Kristo.

Hata hivyo Papa Gregory, akafanya marekebisho na kuanzisha Januari mosi kuwa mwanzo rasmi wa mwaka mpya na si Machi.

Hata pamoja na kutumiwa dunia nzima, zipo baadhi ya kalenda zinazotofautiana na ile ya Papa ambazo ni pamoja na:

### KALENDA YA KIYAHUDI

Huko Uyahudini au Israel leo ni mwaka 5784 wako mbele kwa takribani miaka 3,760 wameshavuka siku nyingi mwaka wa sasa wa 2024.

Wayahudi huadhimisha mwaka mpya mwishoni mwa Septemba, wakati wa mwezi unaoitwa Tishrei. Wanazo kalenda nne tofauti, moja ni kwa ajili ya miti. Tishrei inarejesha kumbukumbu ya kuumbwa kwa ulimwengu.

Kalenda ya lunisolar, inazingatia mzunguko wa jua na mwezi. Ni desturi ya Wayahudi kuzamisha kipande cha tunda katika asali wakati wa mwaka mpya, lakini ni wasaa wa toba na kutafakari maisha yao.




Kalenda ya Kichina ikiwa na mnyama anayewasilisha mwezi. **PICHA : MTANDAO**

> Lakini, Wakorea Kusini pia husherehekea Januari 1 kama mwaka mpya kulingana na kalenda ya Gregorian, iliyopelekwa nchini Korea mwishoni mwa karne ya 19.

### KALENDA YA KICHINA

Kalenda ya Kichina, kama kalenda ya Kiyahudi, ya jadi ya Kichina pia ni ya jua. Na mwaka mpya wa China huangukia tarehe tofauti kila mwaka. Mwaka 2024, kwa mfano, utaadhimishwa Februari 10. Kila mwaka una jina la mmoja wa wanyama 12 katika mchora wa 'zodiaki' wa Kichina.

Mchoro huo una jukumu muhimu katika utamaduni wa China. Mwaka ujao utakuwa wa dragoni. Mwaka mpya wa Kichina pia hujulikana kama tamasha la Spring.

Kunakuwa na likizo ya siku kadhaa ambazo zilianza kuadhimishwa karne zilizopita.

### YA KOREA KUSINI

Mwaka mpya wa Lunar huadhimishwa katika nchi nyingi za Asia, kama vile Korea Kusini. Wakorea Kusini husherehekea mwaka mpya mara mbili.

Siku ya kwanza ya kalenda ya jadi ya Kikorea inaitwa Seollal.

Kama ilivyo nchini China, ni moja ya likizo kubwa zaidi ya mwaka na itaadhimishwa Februari 10 (mwezi ujao).

Lakini, Wakorea Kusini pia husherehekea Januari 1 kama mwaka mpya kulingana na kalenda ya Gregorian, iliyopelekwa nchini Korea mwishoni mwa karne ya 19.

### YA INDIA

Nchini India, miaka mipya mingi. Wahindu katika sehemu tofauti za husherehekea mwaka mpya kulingana na kalenda zao ambazo zinaweza kufuata mzunguko ya jua, mwezi au vyote viwili.

Mwaka Mpya wa Kitamil, ambao huadhimishwa hasa katika jimbo la kusini mwa India la Tamil Nadu, kwa kawaida huwa Aprili 14.

Aidha, unakuwa karibu au tarehe sawa na mwaka mpya wa Kibengali, Kiburma na Kisinhala. Kalenda ya kawaida ya Kitamil inajumuisha mizunguko ya miaka 60.

### KALENDA YA KIAJEMI

Itakumbukwa kuwa mwaka mpya wa Kiajemi huadhimishwa hasa nchini Iran. Kwa Wairani, wako mwaka 1402. Kwa Waajamemi au Wairani mwaka mpya huadhimishwa siku ya kwanza ya msimu wakati mwanga wa jua unapopita katika njia ile ile kwenye vizio vyote viwili, na kuufanya mchana na usiku kuwa na urefu sawa au saa 12 kila mmoja.

Kalenda hiyo inategemea mzunguko wa dunia kuzunguka jua na mwaka mpya au Nowruz, ambayo ina maana ya siku mpya katika Kiajemi, kwa kawaida huangukia karibu na Machi 20.

Nowruz imesherehekewa kwa zaidi ya miaka 3,000 sio tu na Wairani, bali na jamii nyingine pia. Wanaposherehekea wanatayarisha meza iliyopambwa kwa taa saba, na vijana huwatembelea wazee wa familia kwa ajili ya kuwasalimia na kuonyesha heshima.

### YA ETHIOPIA

Wakati nchi nyingi barani Afrika zinatumia kalenda ya Gregorian, Ethiopia sivyo, wana yao inayoitwa Ge'ez. Kwa mujibu wa kalenda yao leo ni mwaka 2016 au 2017.

Wanaiunda kwa kutumia kalenda ya Madhehebu ya Kale ya Kikristo ya Coptic, hivyo iko nyuma ya kalenda ya Gregorian kwa miaka saba hadi minane.

Ni kutokana na hesabu kuwa na utaratibu mbadala wa kuhesabu siku na miezi kulingana na kutangazwa kwa siku ya kuzaliwa Masiha Yesu Kristo.

Kalenda ya Ethiopia ina miezi 12 yenye siku 30 kila mmoja, pamoja na siku tano au sita za ziada (wakati mwingine hujulikana kama mwezi wa 13, ambazo huongezwa mwishoni mwa mwaka ili kulinganisha kalenda na mzunguko wa jua.

Kalenda ya Ethiopia inaeleza kuwa Adamu na Hawa waliishi katika bustani ya Edeni kwa miaka saba kabla ya kufukuzwa. Baada ya kutubu, Mungu aliahidi kuwaokoa baada ya miaka 5,500. Hivyo kwa msingi huo kalenda yao iko nyuma ya Gregorian kwa miaka saba.

Kwa mwaka mpya huitwa kwa Kimahariki 'enkutatash' huadhimishwa Septemba 11 au 12 wakati wa miaka mirefu.

**CHANZO BBC / Mtandao wa Date&Time**



# Prof. Juma: Mahakama ina mchango mkubwa kudhibiti fedha haramu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema Mahakama ya Tanzania ina nafasi kubwa kuimarisha ufanisi katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa tawala za ugaidi.

Alisema hayo jijini hapo wakati akifungua kongamano la siku moja la kujadili masuala ya makosa ya uhalifu wa kifedha lililoandaliwa na Mahakama ya Tanzania kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

Kongamano hilo limefadhiliwa na programu ya kitaifa ya kuzijengea uwezo taasisi za umma zinazohusika na Kuzuia na Kupambana na Rushwa (BSAAT) kwa kushirikiana na washirika.

"Mpango wa Tanzania wa kupambana na utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa kupambana na ugaidi hauwezi kufanikiwa ikiwa Mahakama itakuwa kiungo dhaifu chenye mianya inayoruhusu uhalifu wa kifedha kustawi," alisema.

Alisema kongamano hilo linatoa umuhimu wa maofisa wa mahakama kuendelea kujifunza na kubadilishana utaalamu na uzoefu katika mazingira ya kimataifa ambapo teknolojia zinazobadilika haraka zinafanya ujuzi na utaalamu katika kukabiliana na uhalifu wa kifedha wa kimataifa na kuvuka mipaka.

"Tunakubali wasiwasi unaoongezeka wa kikanda na kimataifa juu ya athari za uhalifu wa kifedha. Uhalifu wa kifedha huyumbisha uchumi wa nchi, siasa, utulivu wa kifedha, maisha na riziki, unakiuka na kupuuza mipaka ya kitaifa na kudhoofisha uchumi wa kimataifa uliounganishwa," alisema.

Alisema katika kongamano hilo pamoja na mambo mengine, washiriki wamejadiliana na kubadilishana uzoefu katika masuala mbalimbali yanayohusiana na vyanzo na athari za makosa ya uhalifu wa kifedha pamoja na njia za jinsi ya kukabiliana na uhalifu huo ambao unazikumba nchi nyingi barani Afrika na dunia kwa ujumla.

Alisema kongamano hilo ni sehemu ya mpango mkakati wa miaka mitano wa mahakama ya Tanzania (2020/2021-2024/25) unaotoa nafasi kwa mahakama kushirikisha wadau katika kutatua changamoto zinazoikumba sekta ya sheria na utoaji haki.

Balozi wa Uingereza Nchini Tanzania, David Concar, alisema kuwa Tanzania na Uingereza zimeshirikiana kwa miaka mingi katika eneo la uhalifu wa kifedha.

"Napongeza nia ya Mahakama ya kuleta wataalamu pamoja kutoka ndani ya Tanzania na kimataifa, kwa kuwa hili ni eneo ambalo linafaidika na majadiliano ya wazi ya changamoto na fursa." Alisema.

Alisema kuwa eneo la uhalifu wa kifedha halisumbui nchini Tanzania pekee bali linawashughulisha hata nchini Uingereza.

"Uingereza ilianza kukabiliana na changamoto hiyo kwa uzito takriban miaka 20 iliyopita, kwa kuanzisha sheria ya kuzipa taasisi zetu mamlaka ya kukabiliana na mapato ya uhalifu. Hata hivyo, kama tunavyojua kupitisha sheria ni hatua ya kwanza tu, changamoto zaidi kufuatilia kupitia mifumo iliyobobea zaidi ya kimataifa na kuzijenga katika kesi za jinai na mashtaka," alisema.

Alisema kuwa kama wafadhili na washirika wa kimataifa wanatamani sana kufanya kazi kwa pamoja na Tanzania katika eneo hilo.

Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na Jaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, Dk. Paul Kihwelo, alisema kuwa kongamano hilo limekuja wakati muafaka ambapo Tanzania iko katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na kikosi kazi cha fedha kufuatia dhamira ya serikali ya kuimarisha ufanisi wa kupambana na utakatishaji fedha haramu na kuhesabu fedha za ugaidi.



Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge kwenye mkutano wa 14 kikao cha tano kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCM yakumbushwa kuteua viongozi waadilifu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, kimetakiwa kuteua wanachama wanaokubalika na wananchi watakaogombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ili kuibuka na ushindi mkubwa.

Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, alisema hayo juzi mkoani hapa, wakati akizungumza na wananchi na wanachama wa CCM katika maadhimisho ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa chama hicho.

Aidha, kabla ya kuzungumza na wananchi alitembelea mradi wa ujenzi wa fremu za chama zinazojengwa uwanja wa mpira wa Liti, Shule ya Msingi ya Dk. Samia, Kituo cha Afya Mtipa na kuweka jiwe la msingi katika ofisi ya CCM Magwanjukim Manispaa ya Singida.

"Tutakuwa na uchaguzi wa serikali za mitaa tumsaidie Mwenyekiti wetu wa CCM Taifa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha tunakwenda kushinda kila kata na vijiji na hilo kinawezekana kwa Singida tunataka mfanye hivyo ili muwe mfano ndani ya Tanzania," alisema. Alisema ili kukiwezesha chama kupata ushindi viongozi waliopo wajipange kuweka mikakati ya kupata wagombea wazuri na kama kuna tofauti zilizopo kwa sasa ziwekwe pembeni.

Maulid ambaye ni mlezi wa CCM katika Mkoa wa Singida alisema ni lazima chana kihakikishe ngazi zote za uongozi kinashinda katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Alisema kuwa endapo CCM itafanya vizuri katika uchaguzi wa serikali za mitaa itakuwa rahisi kwao kushinda tena katika uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025.

Aidha, alitoa wito kwa serikali ya mkoa na chama kuhakikisha wanaendelea kusimamia miradi yote inayotekelezwa kupitia ilani ya CCM inakamilika kwa wakati ili ikifika 2025 kusiwe na deni.

Aliongeza kuwa kupitia maadhimisho hayo ya kuzaliwa kwa CCM Watanzania waendelee kudumisha amani iliyoasisiwa na viongozi wetu, kwani ni dhahiri baadhi ya watu wanaichukia CCM kutokana na uimara na udhubuti wake katika kusimamia amani, upendo na mshikamano nchini.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alisema ushirikiano kati ya chama na serikali mkoani humo ni mzuri ambapo ilani inatekelezwa kikamilifu ili wananchi waweze kupata huduma stahiki.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (MNEC) Mkoa wa Singida, Yohana Msita, alisema katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa mkoa umejipanga kushinda ngazi zote za uongozi kuanzia vitongoji hadi vijiji.

# P2 yatajwa sababu mimba kutungwa nje ya kizazi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MATUMIZI ya vidonge vya kuzuia mimba aina ya P2 yametajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ujauzito kutungwa nje ya nyumba ya uzazi na kuharibu mzunguko wa hedhi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya kinamama wa Hospitali ya Kanda ya Benjamini Mkapa Dodoma (BMH), Dk. Andrew Nyangi, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu madhara ya matumizi ya vidonge hivyo.

Dk. Nyangi, alisema hivi sasa idadi ya watumiaji wa vidonge hivyo imeongeza hususani kwa wanafunzi wa vyuo na wanandoa jambo ambalo linastua sana.

Alisema, wanawake wamekuwa wakitumia vidonge hivyo kama moja ya njia ya uzazi wa mpango lakini hutumia kinyume na maelekezo halisi.

"Kiukweli inashtua sana kuona idadi ya watumiaji wa vidonge vya P2 inaongeza tulichopanga sasa ni kuanza kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi sahihi ya vidonge vya P2," alisema Dk. Nyangi.

Alisema watu wengi wanafanya vidonge hivyo kama njia ya uzazi wa mpango kitu ambacho wanakwenda kinyume na maelekezo ya madaktari namna ya kuvitumia ndani ya saa 72.

Alisema wengi wao wamekuwa wakivitumia ovyo vidonge hivyo ambavyo ni hatari sana kwa afya yao kwa sababu vinaleta madhara.

Kadhalika, alisema hivi sasa wanajipanga kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya matumizi mabaya ya vidonge hivyo kwa ajili ya kuzuia ujauzito.

Alisema watu wengi wanavinunua katika maduka ya dawa bila maelekezo ya daktari na kwenda kuvitumia kadri wanavyojua.

Aliisihi jamii kuacha kutumia vidonge hivyo kiholela badala yake wavitumie kwa maelekezo kamili kutoka kwa daktari anayehusika.

Alisema, vidonge hivyo vinauzwa kwa bei rahisi katika maduka ya dawa na hilo ndilo linachangia wengi kuvitumia kila wanapohisi kushika ujauzito.

Hata hivyo, aliitaka jamii kuonana na daktari endapo wanataka kutumia uzazi wa mpango na si kutumia vidonge vya P2 ili kuzuia ujauzito.





# Ikombe walia na mawasiliano barabara

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

KIJIJI cha Ikombe kilichoko pembezoni mwa safu za Milima ya Livingstone katika mwambao wa Ziwa Nyasa, Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya hakijawahi kuwa na mawasiliano ya barabara tangu kuanzishwa kwake mwaka 1976.

Usafiri pekee wa kuingia na kutoka katika kijiji hicho ni boti na mitumbwi ya asili kupita ndani ya Ziwa Nyasa.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi wa kijiji hicho walisema kuwa kutokana na ugumu wa kusafiri kwenda maeneo mengine hasa Ziwa Nyasa linapochafuka imekuwa ni kero kubwa kwao kwa kuwa shughuli za kiuchumi na kijamii zinakwama.

Sylivanus Gowele ambaye ni mkazi wa kijiji hicho alisema kuwa kukosekana kwa njia nyingine ya usafiri wa kuingia na kutoka kijijini hapo kumekuwa na athari kubwa kwenye maisha yao.

Alisema wakazi wa kijiji hicho wanategemea kupata mahitaji yao muhimu kama vile huduma za kiafya, soko, mashine za kusaga nafaka na elimu ya sekondari katika kijiji cha Matema ambacho ili kukifikia ni lazima kusafiri kupitia ndani ya Ziwa Nyasa.

"Ziwa likichafuka kinamama wajawazito wanaohitaji kwenda kufanyiwa upasuaji kwenye Kituo cha Afya pale Matema hukwama na wengine hupoteza maisha, lakini hata wanafunzi wa sekondari nao hawawezi kwenda shuleni," alisema Gowele.

Kwa upande wake Baraka Lukui ambaye ni mkazi wa kijiji hicho alisema kukosekana kwa barabara inayofika kwenye kijiji hicho kunasababisha hata shughuli za kiuchumi wanazozifanya kutowalipa kwa kuwa hulazimika kuuza bidhaa zao kwa bei ndogo.

"Shughuli za kiuchumi kwenye kijiji chetu ni ufinyazi, kilimo na uvuvi, hata kama tukifanikiwa kuzalisha kwa wingi bidhaa zetu kama vile vyungu, samaki na mazao hatuwezi kuyauza kwa bei kubwa kwa sababu hakuna wateja wanaokuja huku kununua na badala yake tunalazimika kubeba wenyewe kupeleka Matema ambako pia tunauza kwa bei ndogo," alisema Lukui.

Wananchi hao waliiomba serikali kuwajengea barabara mpaka kijijini hapo ili kuwakomboa na kero hizo ambazo wanadai wameishi nazo kwa muda mrefu.

Diwani wa Kata ya Matema, Antony Mwamgunda, alisema licha ya kijiji hicho kuzungukwa na safu za milima ya Livingstone katika upande mmoja na upande mwingine kupakana na Ziwa Nyasa, bado kuna uwezekano wa kujenga barabara kutoka Matema mpaka kijijini hapo kupitia pembezoni mwa safu za milima ya Livingstone.

Alisema udongo wa safu za milima ya Livingstone ni mlaini hivyo ni rahisi kabisa kulima barabara mpaka kwenye kijiji hicho cha Ikombe na ikiwezekana barabara hiyo ikapitiliza na mpaka wilaya ya Ludewa mkoani Ruvuma wanayopakana nayo.

Mwamgunda alisema miaka ya nyuma alitokea padri mmoja wa Kanisa Katoliki ambaye alianza kuhamasisha wananchi kulima barabara hiyo kwa kutumia jembe la mkono, lakini kwa bahati mbaya Padri huyo aliondoka kabla ndoto yake ya kukamilisha barabara hiyo haijatumia.

Akuzungumzia kero hiyo ya wananchi, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase tayari kilio hicho cha wananchi alishakifikisha kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye alishakifanyia kazi.

Alisema Mkuu wa Mkoa wa Mbeya alishamwandikia barua Waziri mwenye dhamana akiomba fedha za ujenzi wa barabara hiyo, ombi ambalo lilikubaliwa.

Alisema baada ya Waziri kukubali ombi hilo, tayari tathmini imeshafanyika na kubaini kuwa shilingi bilioni tatu zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo mpaka kijiji cha Ikombe.

Alisema kwa sasa serikali inatafuta fedha na punde zitakapopatikana ujenzi wa barabara hiyo utaanza mara moja na hivyo kutatua kabisa kero ya wananchi hao..



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Taifa, anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, akizungumza na viongozi wa chama wa Wilaya ya Chunya kwenye eneo inapojengwa ofisi ya chama alipokwenda kukagua maendeleo ya mradi huo, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 47 ya chama hicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafunga siku 43 uchaguzi upite salama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAUMINI wa Kanisa la Moravian Tanzania Ushirika wa Yeriko uliopo katika Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, Jimbo la Kusini Magharibi wamefunga kwa siku 43 wakifanya maombi maalum ya kuliombea taifa lipite salama kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Aidha waumini hao walikuwa wanaliombea taifa lisikumbwe na majanga ambayo yanaweza kusababisha madhara yakiwamo mafuriko, magonjwa na majanga mengine ya asili.

Mchungaji wa ushirika, Paul Mwampamba, ndiye aliyeongoza waumini wa kanisa hilo kufunga alisema Tanzania kama ilivyo kwa mataifa mengine barani Afrika yanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo vita.

Alisema kwenye maombi hayo walimwomba Mungu aliepushe taifa na machafuko ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao za maendeleo kwa amani na utulivu.

Vilevile alisema waliwaombea viongozi wa ngazi mbalimbali wa serikali ili wasifanye uamuzi ambao unaweza kuliingiza taifa kwenye machafuko.

"Lakini pia tuliona yapo mambo mengi maovu yanayolikabili taifa letu yakiwamo mambo ya ushoga na usagaji ambayo sio mazuri kwa taifa letu, hivyo tumemuomba Mungu kwa muda wote huo ili atuepushe na matatizo hayo," alisema Mchungaji Mwampamba.

Akihitimisha mfungo huo, Askofu Mteule wa Kanisa la Moravian Tanzania, Jimbo la Kusini Magharibi, Mchungaji Robert Pangani, aliwataka wanasiasa kutofautiana kwenye itikadi zao bila kuathiri amani ya nchi.

Alisema wanapopishana wanatakiwa wapishane kwa hoja bila kuchochea uvunjifu wa amani kwa kuwa maelezo kuwa upo ushuhuda wa baadhi ya mataifa ambayo yalikuwa kama Tanzania lakini machafuko ya kisiasa yalisababisha yasambaratike.

Alisema amani ya nchi inatakiwa kutunzwa kwa ajili ya ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho huku akiwataka waumini wa kanisa hilo kuendelea kufanya maombi kila wakati ili kulilinda taifa na machafuko.

Nao baadhi ya viongozi walioshiriki ibada ya kuhitimisha mfungo huo waliwapongeza waumini wa kanisa hilo kwa kuamua kuliombea taifa ili liepukane na matatizo mbalimbali.

Diwani wa Kata ya Utengule Usongwe, Yona Ntunjilwa, alisema maombi hayo yaliandaliwa katika kipindi ambacho ni muhimu kwa maelezo kuwa hivi karibuni kutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwakani kutakuwa na uchaguzi mkuu shughuli ambazo alisema zinahitaji maombi.

# TAKUKURU yaonya rushwa uchaguzi serikali za mitaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Njombe imesema itawashughulikia wanasiasa watakaojiingiza kwenye vitendo vya utaoaji rushwa kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Njombe, Cassim Ephrem, aliyasema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi ya miezi mitatu ya kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka 2023 ofisini kwake.

Kamanda Ephrem alisema wanasiasa watakaotafuta madaraka kwa rushwa hawataachwa salama kwa kuwa vitendo hivyo huchangia kuwapo viongozi wasiojali maslahi ya wananchi pindi wanapopata nafasi hizo.

"Ni vema kumwondoa kiongozi ambaye anatoa rushwa kwa maana anawafanya viongozi kuonekana hawasimamii maadili, kama mnajua mwanachama huyu anamwelekeo huu na mnaona taarifa zinaelekea hizi kwa hiyo niwaombe sana viongozi wa chama tusikubali mtu akaharibu taswira ya chama chukueni hatua," alisema Ephrem.

Baadhi ya wananchi mkoani Njombe akiwamo, Gisbert Mgaya walikiri kuwapo kwa vitendo vya rushwa wakati wa chaguzi mbalimbali huku wakitaka hatua kali kuchukuliwa kwa wanaofanya hivyo.

"Wakati wa uchaguzi rushwa uwa inakuwapo kwa sababu kama mimi mpiga kura mgombea wangu ninaona kabisa kiongozi fulani anafaa kuniongoza lakini kwa sababu ya kipengere cha rushwa anakuja mtu mwingine," alisema Mgaya.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga, alisema chama chao kina kanuni na taratibu za kuwashughulikia wale wote wanaotoa rushwa ili wachaguliwe.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA Jimbo la Njombe mjini, Reginard Danda, alisema ni vyema TAKUKURU kafanya kazi kwa uhuru kwani kuna wakati inashindwa kutekeleza majukumu yake.

Inadaiwa kwamba baadhi ya wanasiasa wanatajwa kuanza kutembeza zawadi mbalimbali hivi sasa zikiwamo za fedha, nguo na mablanketi kwa ajili ya kuwarubuni wananchi ili wawachague katika uchaguzi ujazo.





## 19 mbaroni kukutwa na dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATUHUMIWA 19 wamekamatwa katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja baada ya kukutwa na dawa za kulevya kufuatia operesheni iliyofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya Zanzibar, Kanali Nassor Burhani Zubeir, alisema operesheni hiyo pia imekamata jumla ya kilo 125.

Alisema watuhumiwa hao wanashikiliwa na taasisi hiyo kwa mahojiano zaidi huku gari saba zikikamatwa kuhusika na biashara ya dawa za kulevya pamoja na boti mbili pamoja na vifaa vya mawasiliano.

Alisema kiwango cha dawa za kulevya kilichokamatwa ni kikubwa katika historia ya Zanzibar tangu mapinduzi ya mwaka 1964 na ni matokeo ya operesheni kubwa iliyofanywa katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika njia zote ikiwamo baharini.

Kanal Burhan alisema katika kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kilichokamatwa zipo dawa mpya aina ya ''Methamphetamine'' zilizopo katika kundi la vichangamshi sawa na dawa aina ya Kokeini.

''Kiwango kilichokamatwa ni kikubwa ambacho kingefanikiwa kuingia mitaani kingezalisha kete zaidi milioni 6,250,000 wakati idadi ya watu wa Zanzibar ni milioni 1.8,'' alisema.

Aidha alisema wapo baadhi ya watu wanaendelea kusakwa ikiwamo Mzanzibari mmoja ambaye ni mhusika mkuu wa biashara ya dawa za kulevya anayetoa dawa hizo kutoka Pakistani na kuzileta Zanzibar.

''Yupo mfanyabiashara mmoja mkubwa tunamtafuta kwa sababu ndiye mhusika mkuu wa kuingiza dawa za kulevya kutoka Pakistan kuja Zanzibar na Zanzibar haizalishi dawa hizo isipokuwa inatumika kama mlango wa kuingiza dawa za kulevya kutoka nje ya mipaka ya nchi,'' alisema.

Akitoa takwimu alisema hadi sasa bangi inaendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumiwa na wananchi wengi ikiingizwa Zanzibar kutoka mikoa jirani ya Tanzania Bara.

Hata hivyo alisema sheria ya dawa za kulevya namba 8 ya mwaka 2021 inatarajiwa kufanyiwa marekebisho kwa ajili ya kuleta ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Alisema uchunguzi uliofanywa unaonesha kwamba wapo watumishi wa serikali ya mapinduzi Zanzibar wanaojishughulisha katika biashara hiyo sambamba na watendaji wa mahakama na wanasheria.

# Sera mpya Mambo ya Nje kukuza diplomasia uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Mrembo, amesema sera mpya ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imejikita katika dhana ya diplomasia ya uchumi inayohusisha ushiriki wa nchi katika mahusiano ya kikanda na kimataifa kwa kuzingatia maslahi ya kiuchumi.

Aliyasema hayo visiwani humo jana wakati akifungua kongamano la wadau na wananchi wa ukusanyaji wa maoni kuhusu mapendekezo na marekebisho ya sera hiyo ya mwaka 2001.

Alisema serikali inatambua muhimu wa kushirikisha wananchi katika uamuzi unaohusu maslahi yao ya kitaifa na kimataifa na ndio sababu ya Rais Dk. Samia alielekeza kuhakikisha kwamba wadau wa pande mbili za muungano wanashirikishwa kutoa maoni.

Alisema maoni yao ni muhimu katika kuunda sera madhubuti ambayo inawezesha taifa kunufaika ipasavyo na fursa za ushirikiano baina ya Tanzania na mataifa mengine.

"Mtapata fursa ya kuelewa kwa kina masuala muhimu yaliyomo katika sera ya mambo ya nje, aidha kufahamu dhana ya uchumi wa buluu na diplomasia ya uchumi kwa kuzingatia masuala mapya yaliyopendekezwa hivyo kuitumia vizuri fursa hii kwa kujadili na kutoa maoni yenu juu ya masuala mahsusi yatakayoboresha sera hii," alisema.

Aidha, alisema kupitia kongamano hilo serikali itapata maoni na mwelekeo mzuri yatakayowezesha kuboresha sera hiyo kwa kujenga mustakabali mzuri wa vizazi vya sasa na vijavyo.

Waziri huyo alisema sera hiyo inakwenda kuweka matamko ambayo yatabeba matendo na mipango ya nchi yanavyolenga kuendeleza uhusiano wake na nchi zingine. Alisema lazima mipango na matendo hayo ikajielekeze katika kulinda maslahi ya nchi, usalama wa taifa na malengo ya itikadi na mafanikio ya kiuchumi ili kuiendeleza nchi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Januari Makamba, alisema serikali inapotunga sera ni muhimu kupata maoni kwa sababu ni nchi inayoongozwa kwa misingi ya utawala bora.

Alisema sera hiyo ilishakamilika na kupelekwa katika Baraza la Mawaziri kupitishwa, lakini Rais Samia alitaka sera isipitishwe bila ya kupata maoni kwa wadau na wananchi na hivyo kujadiliwa upya na kupata maoni na michango mingi zaidi.

"Tupo hapa kutokana na maelekezo na maono ya Rais Samia ya kutaka kusikiliza maoni ya wananchi na wadau," alisema Waziri Makamba.

Alisema kazi hiyo ya kupitia na kutoa maoni ni muhimu kwa sababu ya sera yenyewe ni nyenzo muhimu ambayo nchi inaitumia katika kujenga mahusiano ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa lengo la kulinda maslahi ya taifa kwa kukuza na kuimarisha uchumi.

Alisema tokea nchi imepata uhuru imejijengea hadhi na sifa duniani kutokana na kuwa na ushawishi mkubwa katika mambo ya kimataifa na yote hiyo imewezeshwa na sera na uongozi mahiri wa viongozi.

Alisema ili kuendeleza kuwa na hadhi, sifa na heshima duniani lazima kutengeneza sera ambayo itaendeleza historia ya nchi ya kuwa na hadhi, sifa na heshima duniani.

Makamba alisema sera hiyo ni muhimu kwa sababu ya malengo ya maendeleo, yataendelea kutegemea ushirikiano wa kimataifa ili kuvutia wawekezaji, kupata mikopo na misaada na kuimarisha jitihada za malengo ya maendeleo ya haraka.

Alisema serikali inafanya maboresho kwa sababu sera iliyopo ni ya muda mrefu takribani miaka 21 na kupitwa na wakati hivyo lazima sera iende na wakati wa sasa.

Alisema sera hiyo ni muhimu katika masuala makubwa yaliohitaji mazingatio ya miaka 21 iliyopita tokea kuanzishwa kwa sera na kwa sasa mambo yamebadilika ikiwamo masuala ya ugaidi, mabadiliko ya tabianchi, uchumi wa buluu, teknolojia na hivyo lazima sera iende na wakati.

"Watanzania wapo wengi waliozaliwa tangu mwaka 2001 mpaka sasa lazima washirikishwe ili kutengeneza Tanzania ijayo," alisema.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Mrembo, akizungumza wakati akifungua kongamano la wadau la kukusanya maoni ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, ambalo limefanyika jana Visiwani Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wahimizwa kupeleka malalamiko Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKILI wa Serikali Mkuu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Hamisa Mmanga Makame, amewataka wananchi visiwani Zanzibar kuandika malalamiko yao na kuyawasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kutafutiwa ufumbuzi.

Wakili Hamisa alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mangapawani Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati wa utoaji wa elimu ya masuala ya kisheria kwa wananchi hao ikiwa ni shamra shamra ya Wiki ya Sheria Zanzibar.

Alisema katika afisi yao lipo faili maalum kwa ajili ya malalamiko ya mwananchi yeyote ili pale anapoyawasilisha, ofisi iweze kuyafanyia kazi malalamiko hayo.

Alisema kuwa, mwananchi atakapoandika malalamiko yake dhidi ya taasisi yoyote ya kiserikali, ofisi ya Mwanasheria Mkuu huchukua jukumu la kuwaita walalamikiwa kwa lengo la kutafuta suluhu dhidi ya malalamiko hayo.

"Mwananchi anapoandika malalamiko yake, sisi tunampa ushauri wa kitaalamu, ikiwa anailalamikia taasisi yoyote ya kiserikali tunachukua jukumu la kuitaarifu taasisi hiyo kwa lengo la kumsaidia mwananchi huyo kupa ufumbuzi," alisema Wakili Hamisa.

Mwananchi wa kijiji hicho, Jafar Said Khamis, alisema shehia yao imegubikwa na changamoto nyingi ikiwamo masuala ya udhalilishaji na migogoro ya ardhi hivyo ni vyema ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuendelea kutoa elimu ili kupambana na changamoto hizo.

"Kwa kweli elimu inahitajika sana. Hapa kuna matatizo mengi, tunaomba kila baada ya miezi mitatu maofisa mje mtoe elimu na kufanya tathmini ya maendeleo yetu kuliko kuja mara moja kwa mwaka," alishauri Jafar.

Naye Ali Juma Nuru aliiomba kujengwa kituo cha polisi kutokana na shehia yao kuwa kubwa na kutawaliwa na harakati nyingi zinazochochea makosa mbalimbali ya kihalifu ikiwamo wizi, udhalilishaji na dawa za kulevya.

Alisema kituo cha polisi kipo masafa ya mbali na hata pale inapotokea kufanyika uhalifu, wananchi hushindwa kumpeleka mhalifu kituoni kutokana na umbali huo.

Sheha wa Shehia ya Mangapwani, Abbas Khamis Maalim, aliipongeza ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuamua kufika katika Shehia yake kutoa elimu ya kisheria ambayo imewanufaisha kwa kiasi kikubwa.

Awali, Wakili wa Serikali Mkuu, kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Said Salim Said, wakati akitoa mada ya udhalilishaji aliwataka wananchi hao kutoa ushirikiano ikiwamo ushahidi pale zinapopelekwa kesi za udhalilishaji mahakamani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZUHURA ISSA RAMADHANI** anatatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye No. **NS0715/0090/2020** kilichotolewa na BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA kupitia Shule ya Sekondari ya ILONGERO mwaka 2020. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **ARU/ARU/RB/405192/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMNE ABDULAZIZI HAMADY anatangaza** kupotea kwa cheti cha kidato cha nne CSEE chenye index namba **S.1327/0007** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI MAZOEZI KLERRUU mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **IRI/IRI/RB/29997/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GRACE AMANI MNANGO** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE300640** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 11/02/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/16705/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NELSON NOAH KIVAMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 967 DUU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/IRI/IRI/1377/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NAOMI JEROME GODBLESS** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **CRV HUNDAI** yenye usajili namba **T 359 AMC,** CHASSIS NAMBA: **RD11103512** na ENGINE NAMBA: **B20B1138743.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/UBU/16795/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CHRISTOPHER ZACHARIA MDUMI** anatangaza kupotea Kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 708 CWT.** aina ya **HAOJUE,** Chassis No. **LC6PCJBJ0M0021286.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/3412/2024**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 26 YA MWAKA 2021**

**DR. GASPER PETER MWEMBEZI ........................................ MDAI**

**VERSUS**

**MARIA WILSON PETER ...................................... MDAIWA 1**

**LUSAKO KILEMBE ................................................ MDIWA 2**

**KWA:** **MARIA WILSON PETER**
**LUSAKO KILEMBE**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 01.03.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa ufike kwa ajili ya kusikiliza Hukumu.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 02 ya mwezi wa **FEBRUARI, 2024**

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
DODOMA

---

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMNISTRATIONAND LOCAL GOVERNMENT**
**MOROGORO MUNICIPAL**
**In reference, please quote:**

**Ref No. MMC/LD/979....................................DATE 31.05.2023**

**YAH; KUSUDIO LA KUTOHUISHA HATI YA KIWANJA NAMBA 3 KITALU T.1 MJI MPYA MANISPAA YA MOROGORO KWA NDUGU SADIKI KASSIM NGUNIKE**

**Mada tajwa hapo juu yahusika,**

Kiwanja namba 3 kitalu T.1 Mji Mpya hapo awali kilitolewa kwa ndugu, **SADIKI KASSIM NGUNIKE wa S.L.P 1321, Morogoro** ambaye aliuza kiwanja hicho kwa **REGISTERED TRUSTEES OF SEVENTH DAY ADVENTIST TANZANIA UNION wa S.L.P 1121, Arusha.**

Kupitia sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Ofisi ya kamishna msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Morogoro haina kusudio la kuhuisha miliki hiyo kwa ndugu SADIKI KASSIM NGUNIKE kwani alikuwa tayari ameuza kiwanja kwa REGISTERED TRUSTEES OF SEVENTH DAY ADVENTIST TANZANIA UNION ofisi inakusudia kuandaa hari kwa REGISTERED TRUSTEES OF SEVENTH DAY ADVENTIST TANZANIA UNION ambao ni wamiliki wa sasa na tayari wameendeleza kiwanja hicho.

Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa kamishna Msaidizi wa Ardhi mkoa wa Morogoro ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya tangazo hili.

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1998 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the Late ANASTAS PIUS GUVETE**

**And**

**In the matter of application for letters of Administration by GLORIA GODSON MSUYA.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have an interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration ) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 01 day of 03 , 2024

Senior Resident Magistrate

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Makanisa yamtupia lawama Rais Ruto

**NAIROBI,** KENYA

BARAZA la Kitaifa la Makanisa nchini Kenya (NCCK) limetoa maoni yao juu ya hali ya taifa hilo huku likishutumu utawala wa Kenya Kwanza kwa kwenda kinyume na ahadi zao walizozitoa kabla ya uchaguzi.

Mkuu wa NCCK, Mchungaji Canon Kinyanjui, juzi alisema utawala wa sasa unaungwa mkono na makanisa na wafuasi wao, licha ya kuieleza serikali inayoongozwa na Rais William Ruto, kwamba wamechoshwa na ushuru unaoongezwa kila uchwao.

"Utawala wa sasa wa Kenya Kwanza uliungwa mkono na kanisa na kwa njia ambayo ni kweli na sahihi. Hata hivyo, waumini wetu wa kanisa wanasema ingawa waliunga mkono Kenya Kwanza, lakini hawakufanya hivyo ili kaongeza ushuru," alisema.

"Pia hawakuipa Kenya Kwanza mamlaka ya kuwatoza ushuru wa nyumba kwa nyumba ambazo hawazihitaji. Pia wanasema, hawataki kushtakiwa zaidi kwa afya kama NHIF inavyoongeza. Pia wanalalamika kuwa wanaona maofisa wa Mamlaka ya Mapato (KRA) wakienda kwenye mashamba yao kuhesabu kuku, nguruwe na punda wao," alisema.

Viongozi hao wa kidini walitoa wito kwa Rais Ruto kutafakari upya sera zake wakisema kuwa hizo za sasa zinawaumiza Wakenya wengi, akieleza kuwa khiyo ndiyo njia pekee ya kupunguza maumivu kwao.

"Sera anazozitekeleza zinaumiza Wakenya, zinazua kilio cha wananchi kutoka tabaka mbalimbali, wananchi wanasema karatasi zao za malipo zimevamiwa kwa njia ambayo haijawahi kuonekana. Wito wetu kwa yeye ni kwamba katika nyakati kama hizi anatakiwa kuwasikiliza wananchi, kubadili mkondo ili maumivu wanayoyapata wananchi yafike mwisho," alisema. **KTN**



# Kuahirishwa uchaguzi kwaibua maandamano nchini Senegal

**DAKAR,** SENEGAL

WANANCHI nchini Senegal wameandamana barabarani kupinga uamuzi wa Rais Macky Sall baada ya kuahirishwa kwa muda usiojulikana uchaguzi mkuu uliokuwa umepangwa kufanyika Februari 25 mwaka huu.

Ilielezwa kuwa katika maandamano hayo yaliyozuka jana nchini humo, polisi walilazimika kutumia mabomu ya machozi kuwasambaratisha waandamanaji katika mji mkuu Dakar.

Pia ilibainishwa kuwa waandamanaji walimiminika barabarani kupinga uamuzi wa miongoni mwa waliokamatwa wakati wa maandamano hayo akiwamo Waziri Mkuu wa zamani, Aminata Touré na Anta Ngom, ambaye ni mmoja wa wagombea urais katika uchaguzi huo.

Wakati wabunge wa shirikisho wakijiandaa kujadili muswaada utakaopitisha uamuzi huo wa Rais Sall, viongozi wa upinzani walitoa wito kwa wananchi kutetea demokrasia huku kukiwa pia na shinikizo la kuwapo kwa mazungumzo na jumuiya ya kikanda ya Afrika Magharibi (ECOWAS).

Pia ilielezwa kuwa katika sakata hilo serikali nchini humo ilisitisha matangazo ya televisheni ya kibinafsi ya Walf iliyokuwa ikirusha maandamano hayo moja kwa moja 'live'.

Kamati ya kimataifa ya kuwalinda wanahabari ililaani hatua hiyo ya serikali na kutoa wito kwa mamlaka za Senegal kuhakikisha kwamba waandishi wa habari wanafanya kazi yao bila vizuizi.

Umoja wa Ulaya (EU) pia ulitoa wito kwa wahusika wote nchini Senegal kushirikiana pamoja kwa ajili ya kuandaa uchaguzi wa haki na uwazi, jumuishi na wa kuaminika haraka iwezekanavyo.

Aidha, msemaji wa Umoja wa Ulaya ambaye anahusika na Sera ya Mambo ya Nje na Usalama, Nabila Massrali, alitoa tamko hilo saa chache kabla ya kuanza kwa maandamano hayo ya upinzani mjini Dakar.

Msemaji huyo wa EU alisema kuahirishwa kwa uchaguzi wa rais nchini Senegal kunaanzisha nyakati za mashaka katika taifa hilo la Afrika.

Rais Macky Sall wa Senegal alitangaza kuahirishwa kwa uchaguzi uliopangwa kufanyika Februari 25, kwa muda usiojulikana, kwa kile alichokitaja kuwa ni kuanzishwa kwa uchunguzi dhidi ya madai ya rushwa miongoni mwa wagombea.

Rais Sall ambaye muhula wake unafikia mwisho Aprili, mwaka huu, na kwamba hakutoa tarehe maalum ya uchaguzi akisema majadiliano ya kitaifa yatafanyika ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru, wa wazi na shirikishi.

Wachambuzi walisema mzozo wa Senegal unaliweka mashakani taifa hilo lenye demokrasia imara hasa kutokana na nchi za ukanda huo kukumbwa na matukio ya mapinduzi ya serikali.

Inabainishwa kuwa Senegal imeingia kwenye mzozo kutokana na mivutano ya kisiasa yenye vurugu baada ya wagombea wa upinzani kunyimwa haki ya kushiriki uchaguzi huo ambao sasa umeahirishwa kwa muda usiojulikana. **DW**




Wananchi nchini Senegal wakikimbia baada ya kutupiwa vitoa machozi na polisi, wakati wa maandamano yaliyozuka kutokana na kuahirishwa kwa uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Februari 25, mwaka huu, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Palestina yaomba mkutano wa amani na Israel

**GAZA,** PALESTINA

RAIS wa Palestina, Mahmoud Abbas, ametoa wito wa kufanyika kwa mkutano wa kimataifa wa amani ili kuhakikisha Israel inaondoka katika maeneo ya Palestina, ikiwamo huko Ukanda wa Gaza inakofanya mashambulizi.

Kiongozi huyo wa taifa la Palestina Abbas alitoa wito wa ulazima wa kufanyika mkutano wa kimataifa wa amani ili kuhakikisha Israel inajiondoa katika maeneo ya Palestina kulingana na maazimio ya uhalali wa kimataifa na ratiba maalum.

Wakati wa mkutano wake na mjumbe wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) katika Mchakato wa Amani ya Mashariki ya Kati, Tor Wensland, alisema kwamba juhudi lazima ziunganishwe ili kuzuia kuhama kwa Mpalestina yeyote kutoka Ukanda wa Gaza.

Maeneo mengine alitaja kuwa ni Ukingo wa Magharibi, ikiwa ni pamoja na Jerusalem Mashariki, kusimamisha mashambulio yote, na kuachilia fedha za Wapalestina kwa ukamilifu.

Rais huyo wa Palestina alisisitiza umuhimu wa kuiwezesha nchi ya Palestina kisiasa na kiuchumi ili iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake kwa wananchi wa Palestina huko Jerusalem, Ukanda wa Gaza na Ukingo wa Magharibi wa Mto Jordan.

Aidha, alitoa wito kwa Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, kuendeleza juhudi zake na kuzidisha juhudi za umoja huo ili kukomesha uchokozi unaoendelea wa Israel dhidi ya watu wa Palestina na kuhakikisha ongezeko la misaada ya kibinadamu na vifaa vya makazi kwa wakazi wa ukanda wa Gaza, haswa katika hali mbaya ya hewa ya sasa.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# KOCHA WA GEITA KUTUMIA DAKIKA 270 KUISOMA SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Geita FC, Denis Kitambi, amesema atatumia dakika 270 sawa na michezo mitatu kuifuatilia na kuisoma Simba kabla ya kukutana nao Februari 12 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kitambi alianza kuwafuatilia wapinzani wake hao kwenye mchezo wao uliopita dhidi ya Mashujaa ya Kigoma na mchezo wa leo ambao Simba wanacheza na Tabora United ni wa pili na baadaye kwenye mchezo dhidi ya Azam FC utakaochezwa Februari 9 kwenye uwanja huo wa CCM Kirumba.

Akizungumza na Nipashe jana, Kitambi alisema anaendelea kukiandaa kikosi chake kulingana na aina ya mchezo, watakutana na Simba hivyo lazima wawe makini na ndio sababu ya kuwafuatilia ili kujua ubora na udhaifu wao.

Alisema licha ya kuwasoma wapinzani wao lakini anaendelea kufanyia kazi mapungufu yaliyopo kwenye kikosi chake baada ya kuyaona kwenye mechi mbili za kirafiki walizocheza hivi karibuni.

"Licha ya kuwafuatilia kwa karibu Simba na sisi tunahitaji kuimarisha timu yetu kulingana na mapungufu yaliyojitokeza katika mechi za kirafiki, kuna makosa tumekuwa tukiyafanya mara kwa mara ikiwamo umakini mdogo kwenye safu ya ulinzi, tunaendelea kufanyia kazi," alisema Kitambi na kuongeza.

"Kwa muda uliopo sasa tunatakiwa kufanyia kazi haraka mapungufu yetu kwa sababu ya ubora wa wapinzani wetu Simba tunaokuja kukutana nao hivi karibuni, ni lazima tuwe kwenye ubora wetu," alisema Kitambi.

Aliongeza kuwa muunganiko wa wachezaji wake umekamilika kwa asilimia 60, bado asilimia 40 ambazo anaimani kabla ya kukutana na Wekundu wa Msimbazi hao katika mchezo wa ligi hiyo atakuwa amepata muunganiko wa asilimia 100.



Vijana wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya michezo Jakaya kikwete jijini Dar es Salaam juzi.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Aisha Mnunka, Stumai kazi ufungaji bora wanawake

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wawili, Aisha Mnunka wa Simba Queens na Stumani Abdallah wa JKT Queens wameendelea kukoleza mbio za kusaka tuzo ya ufungaji bora kwenye Ligi ya Wanawake msimu wa 2023/24, baada ya kila mmoja kufunga bao moja wakiziongoza timu zao kupata ushindi mwishoni mwa wiki iliyopita.

Simba Queens ikiwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma ilipata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Fountain Gate Princess huku Mnunka akifunga bao moja ambalo linamfanya kufikisha jumla ya mabao 10 kwenye orodha ya wafungaji akilingana na Stumai na kuwa vinara wa ufungaji mpaka sasa.

Stumai alifunga bao moja na kufikisha bao la 10 wakati JKT Queens ikiachia kipigo cha nguvu kwa Baobaob Queens cha mabao 6-0 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Mnunka na Stumai, wote ni washambuliaji wa timu ya taifa ya Tanzania ya wanawake, 'Twiga Stars' na kwa sasa wapo kwenye vita ya kuwania ufungaji bora wa Ligi Kuu hiyo ya Wanawake.

Hata hivyo wao wenyewe wamesema wanachoangalia zaidi kwanza ni kuzisaidia timu zao kwenye harakati za kutwaa ubingwa na si kujiangalia wao binafsi.

Pamoja na hayo, washambuliaji hao wana kazi ngumu mbele ya mfungaji bora wa msimu uliopita, Shikangwa ambaye amerejea kwenye kikosi cha Simba Queens na kupachika mabao manne kwenye mechi mbili tu alizocheza.

Mshambuliaji huyo raia wa Kenya, anayeichezea timu ya Taifa ya Wanawake, Harambee Starlets amerejea tena kwenye kikosi cha Simba Queens kipindi cha dirisha dogo la usajili, baada ya kwenda kukipiga kwa muda mfupi kwenye klabu ya Beijing Beikong Women ya nchini China.

Katika mchezo wake wa kwanza alifunga mabao matatu 'hat-trick', Simba Queens ikiibamiza Alliance Queens mabao 7-0, Uwanja wa Azam Complex, na katika mechi ya mwishoni mwa wiki dhidi ya Fountain Gate Princess kwenye ushindi wa mabao 4-0 alifunga bao moja, hivyo kutangaza hali ya hatari kwa Mnunka na Stumai.

## 'Red Eyes' sababu Mlandege kufungwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Msaidizi wa Mabingwa wa Kombe la Mapinduzi, Mlandege FC, Sabri China, amesema kuugua kwa wachezaji wake ugonjwa wa macho maarufu kama 'Red Eyes' ndio sababu ya kufungwa idadi kubwa ya mabao na KVZ FC kwenye mchezo wa kwanza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Mlandege FC juzi ilikubali kipigo hicho ukiwa mchezo wa kwanza tangu walipotwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi mwaka huu baada ya kuifunga Simba bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali uliochezwa Januari 13, Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika mchezo wao dhidi ya KVZ, China alisema wachezaji tisa wa Kikosi cha kwanza wamepata ugonjwa huo wa macho hali iliyo wafanya kuvuruga mipango ya kukipanga kikosi hicho.

Alisema siku nne kabla ya mchezo wao huo idadi ya wachezaji iliongezeka hali iliyopelekea kushindwa hata kuhudhuria mazoezi ya timu ya kujiandaa na mchezo huo muhimu.

Alisema kufungwa mabao mengi kumetokana na kuchezesha wachezaji chaguo la pili ambao wengi wao hawana uzoefu.

## Kocha KenGold FC ataka umakini kubaki kileleni

**Na Oliver Albert**

KOCHA wa KenGold FC, Jumanne Charles, amesema ili kuhakikisha wanaendelea kubaki juu kwenye msimamo wa Ligi ya Championship ni lazima wachezaji wake waongeze umakini hasa kutumia nafasi wanazopata katika michezo yao.

Mechi mbili mfululizo ambazo KenGold imetoka sare dhidi ya Mbeya Kwanza (0-0) na Mbeya City (2-2) ni kama zimewaongezea presha kutoka kwa wapinzani wao wakubwa kwenye ligi hiyo katika mbio za kuwania kupanda daraja.

KenGold FC inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 44, pointi moja zaidi ya Pamba na Biashara United zinazoshika nafasi ya pili na ya tatu.

Katika msimamo huo, Mbeya Kwanza inashika nafasi ya nne ikiwa na pointi 39 wakati TMA ya Arusha inashika nafasi ya tano ikiwa na 38 na zote ziko katika nafasi nzuri katika mbio za kupanda daraja.

Charles alisema anajua kuna presha kubwa nyuma yao lakini jambo ambalo wanatakiwa kulipambania ni kuhakikisha wanaendelea kubaki kileleni.

## ZISIKUPITE

### FERNANDEZ AWANIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia, Al-Hilal iko tayari kufufua nia yake ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United na Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 29, msimu ujao baada ya kushindwa kumsajili Januari. (**Mail**)

### POCHETTINO KUTIMULIWA

KOCHA Mauricio Pochettino yuko katika hatari kubwa ya kutimuliwa baada ya Chelsea kuchapwa 4-1 na Wolves kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumapili. **(Team talks)**

### HODGSON NUSURA ATIMULIWE

MWENYEKITI wa Crystal Palace, Steve Parish, alifikiria sana kumfukuza Roy Hodgson baada ya kushindwa Jumamosi na Brighton, lakini anatatizika kupata mbadala wake ambaye yuko tayari kuchukua nafasi hiyo katika hatua hii ya msimu. **(Guradian)**

### RAPHINHA, FATI WATAKIWA LIVER

LIVERPOOL inavutiwa na winga wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27 na mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 21 kutoka Barcelona kuchukua nafasi ya fowadi wa Misri, Mohamed Salah. **(Teamtalks)**

### ALEXANDER-ARNOLD MKATABA MPYA

LIVERPOOL pia inapanga kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na beki wa kulia wa England mwenye umri wa miaka 25, Trent Alexander-Arnold. **(Football Insider)**

### SESKO KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 20, ambaye analengwa na Chelsea, anaweza kuondoka RB Leipzig msimu wa joto. **(Fotball Transfers)**

### VAN DE BEEK ATEMWA

KLABU ya Eintracht Frankfurt imeamua kutomsajili kiungo Mholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 26, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Manchester United, kwa ajili ya kikosi chao cha Ligi ya Europa. **(Sky Germany)**

### LOOKMAN AWINDWA

WINGA wa zamani wa Everton, Ademola Lookman mwenye umri wa miaka 26, analengwa na Atletico Madrid na Juventus, ambao wanaweza kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, ambaye kwa sasa anachezea Atalanta. **(Sun)**

### BENRAHMA ALIKATALIWA

KLABU ya West Ham ilikataa mpango wa mkopo wa dakika za mwisho mwisho kutoka kwa Fulham kwa winga wa Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 28. **(Fabrizio Romano)**

### HAMILTON KUJIUNGA MAN

NYOTA wa Formula 1, Lewis Hamilton, ambaye atajiunga na Ferrari mwaka 2025, tayari amedokeza kuwa anaweza kuungana na Sir Jim Ratcliffe katika klabu ya Manchester United mara tu pazia la ushirikiano wao na Mercedes litakapofungwa mwaka huu. **(Express)**

### LOKONGA NAFASI NYINGINE

KLABU ya Arsenal inaweza kumpa kiungo wa kati wa Ubelgiji, Albert Sambi Lokonga nafasi nyingine baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kufanya vyema akiwa kwa mkopo Luton Town. **(Football Transfers)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL IMEJIFUNZA KWA MAKOSA - ARTETA

Anaamini kikosi chake kipo imara kwenye kinyang'anyiro cha ubingwa na wamejifunza kutokana na...

**LONDON, England**

KOCHA Mikel Arteta amesema anaamini Arsenal iko imara katika kinyang'anyiro cha kuwania taji la Ligi Kuu ya England na imejifunza somo kutokana na msimu uliopita baada ya kuwalaza vinara Liverpool mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Emirates, juzi Jumapili.

Bukayo Saka alifunga bao la kuongoza dakika ya 14 kabla ya bao la kujifunga la Gabriel katika kipindi cha kwanza kuwaweka sare ya 1-1.

Kujichanganya kati ya Virgil van Dijk na Alisson Becker ulimpa Gabriel Martinelli nafasi ya kuiweka Arsenal mbele dakika ya 67 kabla ya Leandro Trossard aliyetokea benchi kuongeza bao la tatu dakika za lala salama na kuwafanya Arsenal sasa wapitwe pointi mbili dhidi ya Liverpool na kujivuta nafasi ya pili mbele ya Manchester City.

„Tupo pale, hiyo ni hakika," alisema Arteta. Tunataka kuendelea kuwa hapo. Tumekuwa kwenye kiwango bora msimu wote na ndio maana tupo hapa leo.

„Tunachukulia kwa uzito kila mchezo, upatikanaji wa kikosi utakuwa muhimu, tumejifunza kutoka kwenye msimu uliopita, tujaribu kufanya hivyo.

„Ulikuwa mchezo wa ajabu, uchezaji wa ajabu kutoka kwa wachezaji na watu wetu. Hiyo ndiyo mazingira bora ambayo nimeona msimu mzima.

„Tulipambana, tunatakiwa kufanya hivyo, tunapaswa kuwa kwenye kiwango kikubwa kupata mahitaji yetu msimu huu. Nadhani wachezaji walijitoa kwa kila kitu.

„Wanaweka mioyo na roho zao katika kila mpira. Siwezi kujivunia kwa sababu najua jinsi ilivyo ngumu kuifunga timu hii (Liverpool), ni kiasi gani unapaswa kuteseka na ni kiasi gani unapaswa kushughulikia kufanya kile tulichofanya kwenye mpira," alisema Arteta.

Saka aliumia zikiwa zimesalia dakika 11 mchezo kumalizika, lakini Arteta aliwatoa hofu mashabiki kwa kuwa halikuwa tatizo kubwa, lakini aligusia tatizo hilo na kuongeza kuwa suala la utimamu wa mwili lililomfanya Gabriel Jesus kuukosa mchezo huo litamweka nje kwa „siku kadhaa".

# MISRI YAMTIMUA KOCHA WAKE

**CAIRO, Misri**

MISRI imemtimua Rui Vitoria kama kocha mkuu wiki moja baada ya kuondolewa kwenye hatua ya 16 bora ya michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon.

Misri imemfuta kazi kocha huyo raia wa Ureno kufuatia kampeni yao ya kusikitisha ya Kombe la Mataifa ya Afrika nchini Ivory Coast.

Mafarao walitoka katika michuano hiyo katika hatua ya 16 bora baada ya kufungwa kwa mikwaju ya penalti 8-7 dhidi ya DR Congo mjini San Pedro.

Misri hawakuwa kwenye kiwango bora katika michuano hiyo na hawakushinda mchezo wowote.

Pia walikumbwa na jeraha la mapema la nahodha wao, Mohamed Salah.

Misri walitoka sare tatu mfululizo za 2-2 katika hatua ya makundi - dhidi ya Msumbiji, Ghana na Cape Verde - kabla ya kuondolewa na DR Congo.

Katika taarifa ya Jumapili, Shirikisho la Soka la Misri (EFA) lilisema Vitoria mwenye umri wa miaka 53 na wafanyakazi wake wote wamefukuzwa kazi baada ya mkutano wa bodi ya wakurugenzi.

Mohamed Youssef, kocha wa zamani wa Al Ahly, ameteuliwa kuwa kocha wa muda wa Misri ingawa EFA imesema "pia tutaangalia CV za baadhi ya makocha wa kigeni."

Aliyekuwa Kocha wa Benfica na Spartak Moscow, Vitoria aliteuliwa kuwa kocha mkuu wa Misri mwaka 2022, akimrithi Ehab Galal.

Alisaini mkataba wa miaka minne ambao ungemfikisha kwenye Kombe la Dunia la 2026.

Utawala wake na Mafarao ulianza vizuri, akishinda michezo 12 kati ya 14 kabla ya kuanza kwa Afcon.

Hii ilijumuisha ushindi wao mara mbili mwanzoni mwa kampeni ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la 2026.

Kufukuzwa kwa Vitoria kunafuatia kuondoka kwa makocha wengine kadhaa kwenye Afcon.

Kocha wa Algeria, Djamel Belmadi, Tom Saintfiet wa Gambia, Chris Hughton wa Ghana, Jalel Kadri wa Tunisia na Kocha wa Ivory Coast, Jean-Louis Gasset wote waliachana na timu zao.



# Jeraha la Martinez lamtia hofu Ten Hag

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema anahofia hali mbaya zaidi baada ya Lisandro Martínez kupata jeraha la goti wakati wa ushindi wa 3-0 dhidi ya West Ham, Jumapili.

Martínez alilazimika kutolewa nje kipindi cha pili baada ya beki wa West Ham Vladimír Coufal kuangukia mguu wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina.

Awali beki huyo wa kati wa United alijaribu kuendelea lakini alishindwa na nafasi yake kuchukuliwa na Raphaël Varane.

Ten Hag aliita jeraha hilo kuwa "janga binafsi" kwa Martínez, ambaye alikuwa anaanza kwa mara ya tatu baada ya kuwa nje kwa zaidi ya miezi minne kutokana na jeraha la mguu.

"Siwezi kusema ni mbaya kiasi gani, lakini haionekani kuwa nzuri kwa hiyo kuna wasiwasi mkubwa," alisema Ten Hag.

"Inabidi tusubiri siku zijazo kwa uchunguzi ndipo tunaweza kukuambia zaidi. Tunafanya kila kitu kupata uchunguzi sahihi ili kuona ni kiasi gami ameumia.

"Ana huzuni sana, amekata tamaa sana.



Tuko naye. Ni janga binafsi. Tusubiri lakini ni mbaya sana."

Jeraha kwa Martinez ndilo lililosababisha hasara pekee kwa United siku ambayo waliandikisha ushindi wao mkubwa zaidi wakiwa nyumbani kwenye michezo ya ligi kwa msimu huu.

Kwa mara ya kwanza msimu huu, timu ya Ten Hag ilishinda mchezo wa Ligi Kuu kwa zaidi ya tofauti ya bao moja kutokana na bao la nne la Rasmus Højlund katika michezo yake minne iliyopita na mawili kutoka kwa Alejandro Garnacho.

"Ni mchezo mmoja tu, kwa hiyo usisherehekee sana," alisema Ten Hag.

"Hatuna sababu za kufanya hivyo lakini kwa leo (juzi) tumefurahishwa na hilo, sasa tuwe na timu ambayo ipo kwenye usawa uwanjani, tunaweza kucheza vizuri zaidi lakini pia unaona maendeleo yanakuja.

"Sio kuhusu mchezaji mmoja, ni kuhusu timu. Ndivyo nimeona leo (juzi). Ilionekana kama timu. Kumi na moja wakilinda, kumi na moja wakishambulia. Kwangu, ilikuwa ya kufurahisha kutazama."

## Kocha Nigeria ataka mabao zaidi

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KOCHA wa Nigeria, José Peseiro ametoa wito kwa timu yake kutumia vizuri nafasi za kufunga licha ya kujivunia safu kali ya ulinzi kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon, inayoendelea nchini Ivory Coast.

Super Eagles wametinga nusufainali baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Angola ambao walicheza mchezo wao wa nne mfululizo bila kuruhusu bao kwenye mashindano hayo.

Nigeria imetinga nusu fainali ya michuano hiyo na sasa itacheza na Afrika Kusini kesho Jumatano.

Kocha huyo na wachezaji wake sasa wamebakisha mechi mbili kabla ya Nigeria kupata taji lake la nne la mashindano hayo.

Huku akisifu uimara wa ulinzi wa Nigeria, Peseiro anatumaini kuona maboresho katika safu ya ushambuliaji.

"Kwa mara nyingine tena tulicheza bila kufungwa, tukafunga bao, lakini ningependa zaidi. Timu itengeneza nafasi nyingi zaidi," alisema.

Akiwa na mabao sita pekee katika michezo mitano, Mreno huyo anahisi Nigeria haitumii ubora wao.

"Sisi ni timu yenye ubora, Angola ilikuwa nzuri sana, lakini tulikuwa na bahati zaidi. Ninaendelea kuridhika na wachezaji wangu lakini nataka tuwe na ufanisi zaidi," aliongeza Peseiro.

Kocha huyo alikiri kwamba safu ya ushambuliaji haijasaidiwa sana kutokana na kukosekana wachezaji ambao ni majeruhi.

"Tunakosa baadhi ya wachezaji kama Iheanacho na Aribo, kwa hiyo imekuwa ngumu. Lakini wengine lazima sasa waongeze nguvu," alibainisha.

Huku Nigeria ikifukuzia taji la nne la Afcon, Peseiro anajua kuwa kupata makali ya kiafya kunaweza kuwa muhimu.

Ushindi dhidi ya Afrika Kusini siku ya Jumatano katika Uwanja wa Paix mjini Bouaké utawaleta karibu na lengo hilo muhimu.



# SERENGETI GIRLS YANOA MAKALI 'KUPINDUA MEZA'

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 17 ‚Serengeti Girls', Hilda Masache, amesema wanafanyia kazi maeneo mawili ili kusaka makali yatakayowawezesha kupindua meza mbele ya Zambia wakati wa mchezo wao wa marudiano wa kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Zambia.

Serengeti Girls ina kibarua kigumu kwenye mchezo huo wa marudiano utakaochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex baada ya mchezo wa kwanza kukubali kipigo cha mabao 5-0 wakiwa ugenini Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Hilda alisema kiufundi mambo mawili yalichangia ikiwamo safu yake ya ulinzi kufanya makosa kulikosababisha kupoteza kwa idadi kubwa ya mabao.

Alisema kulikuwa na makosa kwenye kukaba na wapinzani wao hao walitumia nafasi hiyo hasa mipira mirefu ambayo waliidondosha nyuma ya safu ya ulinzi na kufanikiwa kupata ushindi huo mkubwa unaowafanya Serengeti Girls kuwa na kazi kubwa kuweza kusonga mbele.

"Tumepoteza kwa idadi kubwa ya mabao, pia safu ya ushambuliaji tulipata nafasi lakini tulishindwa kuzitumia, hayo ni maeneo muhimu yalikuwa na shida, kwa saa tunafanyia kazi kurekebisha mambo kabla ya mchezo wetu wa marudiano," alisema Hilda.

Aliongeza kuwa wanahitaji kufanyia kazi na kusahihisha mapungufu yao haraka kabla ya mchezo wa marudiano ambao watakuwa nyumbani kuweza kufunga idadi ya mabao zaidi ya tano waliyofungwa.

Katika hatua nyingine Ofisa Habari wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema Ligi ya Wanawake imesimama kwa muda na wiki hii wanatarajia kutangaza kikosi cha timu ya wakubwa ya wanawake 'Twiga Stars' ambayo inakabiliwa na mechi ya kufuzu michezo ya Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini.

"Tunatarajia kuwa na mechi dhidi ya Afrika Kusini ya kufuzu Olimpiki, wiki hii baada ya mechi za wikiendi iliyopita ligi imesimama na Kocha Mkuu, Bakark Shime, atatangaza kikosi kwa ajili ya mechi yetu hiyo itakayochezwa Februari 19, mwaka huu, tukianzia ugenini," alisema Ndimbo.




Mmoja wa washindi wa promosheni ya 'Soka la Afrika Limeitika' Enock Charles (katikati), akiwa ameshikilia mfano wa tiketi ya kwenda Ivory Coast kushuhudia Nusu Fainali za AFCON, kushoto ni Meneja wa Bidhaa za Ongezeko la Thamani wa Tigo, Adam Francis, kulia ni Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Green Telecom wanaoshirikiana na Tigo kuendesha promosheni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanne kushuhudia nusu fainali AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wa nne wa promosheni ya ‚Soka la Afrika Limeitika' wameagwa jana tayari kwa safari ya kwenda Ivory Coast leo kushuhudia michezo ya nusu fainali ya Fainali za Afrika (AFCON) inayoanza kesho kwa Afrika Kusini kucheza na wenyeji Ivory Coast na Nigeria kuumana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Washindi hao, Dickson Michael kutoka Arusha, George Dilunga wa Tanga, Enock Charles kutoka Zanzibar na Deodatus Sagamiko wa Dar es Salaam waliagwa jana kwenye ofisi za Tigo wanaoendesha promosheni hiyo kwa kushirikiana na kampuni ya Green Telecom.

Akizungumza wakati wa kuwaaga washindi hao, Meneja wa Bidhaa za ongezeko la Thamani wa Tigo, Adam Francis, alisema kampeni hiyo inashirikisha wateja ambapo wanapata fursa ya kujibu maswali kwenye simu na kujiweka katika nafasi nzuri ya kushinda.

Alisema zawadi wanazotoa ni pamoja na pesa mpaka Shilingi milioni 10 pamoja na zawadi nyingine zikiwamo safari ya kwenda kushuhudia fainali hizo za Afcon.

„Promosheni hii inaendelea na wateja wa tigo waendelee tu kujibu maswali baada ya kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwenda namba 15670, maswali ni rahisi sana kwa wapenda soka, leo tunawaaga washindi wetu hawa ambao wanaenda Ivory Coast kwa gharama zilizolipiwa," alisema Francis.

Mmoja wa washindi hao Deudatus Sagamiko alisema, amefurahishwa na kupata mshangao mkubwa kupata nafasi hiyo ya kwenda Ivory Coast kushuhudia michezo hiyo ya nusu fainali ya AFCON.

Alisema wateja waendelee kushiriki katika promosheni hiyo inayoendelea ili kujiweka katika nafasi ya kushinda zawadi mbalimbali.

„Promosheni hii siku ya mwisho kuna mshindi wa milioni 10, ni vizuri kama watu wataendelea kushiriki promosheni hii," alisema Sagamiko.

Washindi hao watakuwa nchini Ivory Coast kwa siku tatu na kupata fursa ya kushuhudia mechi zote za nusu fainali na wanatarajiwa kuondoka leo.



## Simba SC kuwashangaza Tabora United

INATOKA UK. 24

sho (leo)," alisema Matola.

Kwa upande wake, Kocha wa Tabora United, Goran Kopunovic, alikiri mchezo huo hautakuwa mwepesi kwa timu yake kutokana na uimara wa Simba lakini wapo tayari kupambania pointi tatu.

"Hii ni mechi ngumu, tunaenda kupambana, hatuna presha, hatuiogopi Simba kwa sababu wote tunacheza na wachezaji 11 , tumejipanga vizuri ingawa tutacheza kwa kuwaheshimu wapinzani wetu, tunahitaji alama tatu mechi hii na zingine zilizopo mbele yetu," alisema Goran.

Alisema watawapa heshima yao Simba kama moja ya timu bora na kubwa nchini, lakini uwanjani watapambana kuhakikisha wanapata pointi tatu wakiwa kwenye uwanja wao wa nyumbani.

## Yanga kuzindua ofisi mpya Dar

INATOKA UK. 24

kutano kwa wanahabari, ambapo pia kutakuwa na vitendea kazi kwa waandishi kama kompyuta mpakato na kamera, lengo ni kuwarahisishia kazi zao pindi wanapokuja kwenye mikutano," alisema Kamwe.

Hii si mara ya kwanza kwa klabu hiyo kufanya ukarabati wa jengo hilo ambapo mara kwa mara imekuwa ikifanya hivyo baada ya miaka kadhaa na kulifanya kuendelea kuvutia ndani na nje.

Awali Makao Makuu ya Yanga yalikuwa Mtaa wa Mafia na Nyamwezi, Dar es Salaam, jengo lililojengwa katikati ya miaka ya 1960 chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa wakati huo, Kitwana Kondo na Katibu Mkuu Jabir Katundu.

Hata hivyo, ilipofika mwishoni mwa miaka hiyo, viongozi waliona Yanga inahitaji Makao Makuu yenye hadhi zaidi ya waliokuwa nayo, hivyo kuamua kufunga safari kwenda kwa Rais wa Zanzibar na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Abeid Amani Karume, kumwomba ufadhili ambapo kwa kiasi kikubwa ndiye aliyefanikisha kujengwa kwa makao makuu ya klabu hiyo Mtaa wa Twiga na Jangwani ambayo kesho yatazinduliwa baada ya ukarabati mkubwa uliofanywa.

Michezo
Jumanne Februari 6, 2024
Nipashe

## Misri yamtimua kocha wake

UKURASA 22



UKARABATI...




Jengo la Yanga kabla ya ukarabati. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA KUZINDUA OFISI MPYA DAR

●●●Ni baada ya ukarabati mkubwa kwenye jengo la klabu hiyo, sasa kila idara kuwa na ofisi yake huku kukiwa na...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI jana wakishuhudia timu yao ikicheza na Dodoma FC jijini Dodoma, kesho uongozi wa klabu ya Yanga utazindua rasmi ofisi za klabu hiyo zilizoko ndani ya jengo la makao makuu baada ya kufanyika ukarabati mkubwa.

Yanga inazindua ofisi hizo ambapo sasa kila idara itakuwa na ofisi zake huku pia wakijenga ukumbi wa kisasa wa mikutano ukiwa na vifaa vyote vya kisasa kuwawezesha waandishi wa habari na watu wengine kufanya shughuli zao kirahisi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema uzinduzi huo unafanyika ili ofisi za klabu hiyo ziendane na hadhi na sifa ya klabu yao waliyonayo barani Afrika.

Kamwe alisema ukarabati huo wa ofisi umezingatia mahitaji muhimu hasa kwenye soka la kisasa ambapo vitu vingi vimeongezwa na kufanya kuwa ofisi za kisasa zinazofanana na ofisi za klabu nyingine kubwa Afrika.

"Tumefanya ukarabati wa kihistoria, tumekuwa moja ya klabu yenye ofisi bora ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ukarabati huu umefanywa na uongozi huu uliopo madarakani ambao umechaguliwa na wanachama, Jumatano tutazindua ofisi na makao makuu yetu mapya chini ya rais wa klabu yetu, Injinia Hersi Said," alisema Kamwe.

Alisema katika jengo hilo lililokarabatiwa kwa kiwango kikubwa pia kutakuwa na ofisi ya masoko, ofisi ya watu wa sheria, ofisi za viongozi wa juu wa klabu hiyo kila mmoja akiwa na ofisi yake.

"Tumetengeneza chumba cha mi-

INAENDELEA UK. 23

## Simba SC kuwashangaza Tabora United nyumbani

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema licha ya kufahamu kuwa mchezo wao wa leo dhidi ya wenyeji wao Tabora United kutarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa, lengo lao litabaki palepale kupambana na kuvuna alama tatu muhimu.

Matola amesema ushindi walioupata kwenye mchezo uliopita dhidi ya Mashujaa wakiwa ugenini utakuwa chachu kwao kusaka ushindi leo ili kuendelea kukoleza mbio zao za kuwania ubingwa msimu huu.

Alisema licha ya Tabora United kuwa nyumbani, watapambana kuhakikisha wanawashangaza kwa kuwafunga mbele ya mashabiki wao.

Simba ambayo mechi iliyopita walimkosa kiungo wao, Fabrice Ngoma ambaye alienda kwao kutatua matatizo ya kifamilia amerejea na jana ameungana na kikosi cha timu hiyo na uwenda kocha akamtumia leo.

Wakati Tabora United mechi yao ya mwisho na Yanga waliocheza Desemba 23, mwaka jana kwa kuruhusu bao 1-0 waliocheza uwanja huo wa Ally Hassan Mwinyi, kikosi cha Tabora United kinachonolewa na Goran Kopunovic aliyekuwa kocha wa zamani wa Simba.

"Haitakuwa mechi rahisi, tumeangalia michezo yao ni timu ngumu, lakini pamoja na yote tunahitaji pointi tatu kutoka Tabora United, wachezaji wote wapo kwenye hali nzuri na tunategemea kupata upinzani mkubwa lakini tumejipanga kuhakikisha tunashinda," alisema Matola.

Kuhusu Ngoma kucheza au kutocheza mechi ya leo, kocha huyo alisema kiungo huyo ameungana na wenzake jana na mipango yao kama benchi la ufundi wataangalia kumpa nafasi au laa, kutokana na aina ya mchezo wa wapinzani wao.

Kuhusiana na ugumu wa ratiba ya michezo ya Ligi Kuu na Kombe la FA, Matola alisema hawapaswi kulalamika bali kupambana katika kila mchezo kuweza kupata ushindi ili kufikia lengo lao.

"Ni kweli ratiba ni ngumu, lakini hii si kwa Simba tu, tumejipanga vizuri na tutapambana kuhakikisha hatupotezi pointi, tupo tayari kwa mchezo wa ke-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042